**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

| | | |
|---|---|---|
| **MHE. ZUBEIR ALI MAULID** | **-** | **SPIKA** |
| 1. Mhe. Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake |
| 2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani |
| 3. Mhe. Shehe Hamad Mattar | - | Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda |
| 5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka |
| 6.Mhe. Haji Omar Kheri | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu |
| 7. Mhe. Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi |

| | | |
|---|---|---|
| 8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge |
| 10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | - | MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 11. Mhe. Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake |
| 12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali | - | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais |
| 13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume | - | MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. Rashid Ali Juma | - | MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani |
| 15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais |
| 16. Mhe. Maudline Cyrus Castico | - | MBM/Waziri wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais |
| 17. Mhe. Salama Aboud Talib | - | MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake |
| 18. Mhe. Juma Ali Khatib | - | MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais |
| 19. Mhe. Said Soud Said | - | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais |
| 20. Mhe. Khamis Juma Mwalim | - | Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe |
| 21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera |
| 22. Mhe. Shamata Shaame Khamis | - | Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni |

| | | |
|---|---|---|
| 23. Mhe. Harusi Said Suleiman | - | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete |
| 24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri | - | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani |
| 25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi |
| 26. Mhe. Chum Kombo Khamis | - | Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake |
| 27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake |
| 28. Mhe. Lulu Msham Abdalla | - | Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake |
| 29. Mhe. Juma Makungu Juma | - | Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini |
| 30. Mhe. Abdalla Ali Kombo | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani | - | Jimbo la Jang'ombe |

| | | |
|---|---|---|
| 32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil | - | Uteuzi wa Rais |
| 33. Mhe. Ali Khamis Bakar | - | Jimbo la Tumbe |
| 34. Mhe. Ali Salum Haji | - | Jimbo la Kwahani |
| 35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) | - | Jimbo la Kijitoupele |
| 36. Mhe. Ame Haji Ali | - | Jimbo la Nungwi |
| 37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Kiwengwa |
| 39. Mhe. Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid | - | Jimbo la Wawi |
| 42. Mhe. Hamida Abdalla Issa | - | Nafasi za Wanawake |
| 43. Mhe. Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Shaurimoyo |
| 44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 45. Mhe. Hidaya Ali Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) | - | Jimbo la Mtoni |
| 47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub | - | Jimbo la Paje |
| 48. Mhe. Khadija Omar Kibano | - | Jimbo la Mtambwe |
| 49. Mhe. Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti | - | Jimbo la Mtopepo |
| 51. Mhe. Makame Said Juma | - | Jimbo la Kojani |
| 52. Mhe. Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi

72. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu

73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake

| | | |
|---|---|---|
| 74. Mhe. Salma Mussa Bilal | - | Nafasi za Wanawake |
| 75. Mhe. Shaib Said Ali | - | Jimbo la Chonga |
| 76. Mhe. Simai Mohammed Said | - | Jimbo la Tunguu |
| 77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya | - | Uteuzi wa Rais |
| 78. Mhe. Suleiman Makame Ali | - | Jimbo la Ziwani |
| 79. Mhe. Suleiman Sarahan Said | - | Jimbo la Chakechake |
| 80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi | - | Nafasi za Wanawake |
| 81. Mhe. Ussi Yahya Haji | - | Jimbo la Mkwajuni |
| 82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir | - | Nafasi za Wanawake |
| 84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi | - | Jimbo la Fuoni |
| 85. Mhe. Zaina Abdalla Salum | - | Nafasi za Wanawake |
| 86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar | - | Nafasi za Wanawake |

| | | |
|---|---|---|
| Ndugu Raya Issa Msellem | - | Katibu wa Baraza la Wawakilishi |

**Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 09 Juni, 2017**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

## DUA

*Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua*

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kuwasilisha mezani kauli ya Serikali kuhusiana na Skuli ya Darajani na Vikokotoni katika uendelezaji wa Ukanda wa Darajani maarufu *(Darajani Corridor).* Naomba kuwasilisha.

## KAULI ZA SERIKALI

**Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, Kauli ya Serikali kuhusiana na Skuli ya Darajani na Vikokotoni katika uendelezaji wa Ukanda wa Darajani. Kauli hii imetayarishwa chini ya kanuni 43(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, wakati wa kujadili bajeti na kupitisha vifungu vya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar kulijitokeza hoja ya kuiomba serikali kufikiria kubadilisha maamuzi ya kuivunja Skuli ya Vikokotoni wakati utakapoanza ujenzi wa uendelezaji ukanda wa Darajani au *Darajani Corridor* ili kuitunza historia ya majengo hayo.

Mhe. Balozi Ali Karume ambaye ni Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji wakati akijibu hoja hizo aliahidi Baraza lako tukufu kuwa atalifikisha suala hilo serikalini kwa mashirikiano zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa mashauriano hayo yamefanyika serikalini na maoni yaliyotolewa hapa yameonekana na uzito wake. Lakini ukilinganisha na faida ambayo itapatikana kutokana na mpango huo ambao ulipitishwa na serikali na sasa unasubiri utekelezaji tu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona ni vyema kuendelea na maamuzi yake ya hapo awali ambayo ni kuivunja Skuli ya Vikokotoni na kujenga majengo makubwa ya kibiashara.

Skuli ya Darajani ambayo ndio ya kihistoria haitovunjwa bali itabadilishwa matumizi kuendana na mpango mpya wa matumizi ya eneo hilo. Utaratibu tayari unaandaliwa ili wanafunzi wanaosoma katika skuli hizo watajengewa skuli ya mpya ya kisasa kwenye eneo la Rahaleo na fedha za ujenzi huo tayari zimepatikana kutoka mfuko wa *OPEC Fund*.

Mhe. Naibu Spika, serikali ina jukumu la kuwapatia watoto wetu sehemu bora zaidi ya kusomea ili wapate elimu, kwani elimu ndio msingi wa maendeleo ya nchi yoyote duniani. Ndio maana Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohamed Shein amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa kila mtoto wa Zanzibar anapata fursa ya kusoma na katika mazingira mazuri ya kuwapatia skuli bora na zenye madarasa ya kutosha, madawati ya kutosha, vitabu vya kutosha na walimu waliohamasika kuwafunza vijana wetu.

Aidha, tangu Mapinduzi yetu Matukufu ya mwaka 1964 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Chama cha *Afro Shirazi Party* na sasa Chama cha Mapinduzi moja kati ya vipaumbele vyake muhimu ni elimu. Kwa misingi hiyo Mhe. Naibu Spika, ndio maana serikali inajiandaa kuwapatia wanafunzi wa skuli hizo majengo mapya na ya kisasa ili waendelee na masomo kwa utulivu, tafauti na eneo la Darajani ambalo kuna vurumai za watu na kelele ambazo zinawaondolea wanafunzi na walimu utulivu wanaohitaji katika mazingira ya kujifunza.

Mhe. Naibu Spika, natumai sasa suala hili limeeleweka vyema kwa nini serikali imeamua kulivunja jengo la serikali la Skuli ya Vikokotoni na ni matumaini yangu kuwa suala hili halitoibuka tena Barazani hapa. Niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wa Baraza lako tukufu tuunge mkono mipango ya serikali katika kubadili mji wetu wa Zanzibar ili uwe wa haiba nzuri na kuvutia ili sisi wenyewe na wageni tuone fahari ya kuwa na mji wenye mipangilio bora kwa majengo na shughuli zinafanyika kwa utaratibu mzuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana tunakushukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa taarifa yako.

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Kuhusu utaratibu.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa nilikuwa sijamaliza kuzungumza wacha nimalize kuzungumza nilikuwa nampongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa taarifa yake. Sasa naomba kuhusu utaratibu uje. Mhe. Mohammed Said Mohammed. (*Makofi*)

## UTARATIBU

**Mhe. Mohammed Said Mohammed:** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kauli ya serikali aliyoitoa na mimi naungana moja kwa moja bila ya kuipinga chochote.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa nataka tu kifungu alichokitumia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kifungu cha 43(3) cha kuwasilisha hoja. Lakini nataka sasa nitilie mkazo kifungu cha 147 ili sasa tuweke kando kanuni hiyo aliyoitaja Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na

kuweza kujadili kwa upana wake kauli hii, ili basi tuweze kuona umuhimu wa jambo lenyewe ambalo vijana wengi wamesoma pale akiwemo Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ili basi tuone kwa upana wake kulijadili jambo hili. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Said Mohammed amekaribia kunifilisi au nasema kanifilisi. Hii kanuni haiko upande mmoja tu, hii kanuni iko kama shilingi, iko sehemu mbili unaweza kugeuza huku na huku, mimi natia msisitizo wa suala hilo alilolisema mkuu wangu Mhe. Mohammed Said Mohammed. Kwa hivyo, hoja ijadiliwe ili wananchi waelewe ukweli wa kadhia hii ilivyo.

Maana yake hapa kuna *hansard* ya Mhe. Ali Abeid Karume na aliyotoa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi ni vitu viwili tafauti na mawaziri wanafanyakazi kwa niaba, sasa tuijadili tupate kujua ukweli au kama utaniruhusu niisome nitasoma ninayo hapa. Sasa sijui tushike wapi inaonekana hili jambo halijapangwa vizuri.

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa umemaliza?

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Nimemaliza Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Haya naomba ukae, Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf ulisimama.

**Mhe. Nadir Abdul- Latif Yussuf:** Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa naingia sijasimama.

**Mhe. Naibu Spika:** Haya kaa kitako sawa. Waheshimiwa Wajumbe nimesikia hoja zenu na kama nilivyoelezea kutokana na kanuni ambazo mmezitaja iko nafasi lakini ni ndogo sana nyembamba sana ya kuweza kulijadili suala hili. Lakini hiyo haina maana kwamba tuweze kuiacha kanuni ambayo inatupa

nafasi ya kuuliza maswali. Kanuni hii ina nguvu zaidi kuliko hizo ambazo mnazitaja nyinyi Waheshimiwa na kwa kuwa mmekipa kiti mamlaka ya maamuzi nasema hivi kwamba tuendelee kutumia kanuni ya 43(3) kwa ajili ya kuuliza maswali kutokana na taarifa hiyo.

Nafikiri hilo limeeleweka na tunaendelea. Waheshimiwa tunaendelea anayetaka kuuliza swali Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Samahani kwanza naanza na Wenyeviti. Nimepewa taarifa Wenyeviti wawili watakuwa wana taarifa zao baada ya hapo ndio watauliza maswali. Mhe. Jaku Hashim Ayoub subiri mpaka zimalizike taarifa za Wenyeviti. Mhe. Hamza Hassan Juma.

**Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano):** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi kuweza kutoa maoni kuhusu Kauli ya Serikali juu hatma ya Skuli ya Darajani na Skuli ya Vikokotoni katika uendelezaji wa Ukanda wa Darajani.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu tumekaa pamoja kwamba tumepata muda mfupi sana wa kuipitia kauli hii ya serikali lakini tumejaribu kuchukua uzoefu. Lakini vile vile tukajaribu kutafuta maoni mbali mbali ya kitaalamu ili kuweza kuishauri vizuri serikali yetu.

Mhe. Naibu Spika, nia ya serikali yetu ni nzuri sana na kwa kweli ina haja ya kuungwa mkono katika kubadilisha Ukanda wa Darajani kuwa ni ukanda wa biashara na kubadilisha matumizi ya zile skuli zetu mbili ambazo ziko katika urithi wa kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu maoni ya kamati. Maoni ya Kamati Mhe. Naibu Spika, sisi kama Zanzibar tumekubali wenyewe kuuweka mji wetu wa Zanzibar *Stone town* kuwa ni urithi wa kimataifa na tumekuwa tukishirikiana sana na *UNESCO*

tumeweza kupata misaada mbali mbali kupitia *UNESCO*. Lakini vile vile tuweza kuulinda Mji Mkongwe usiharibiwe ile hadhi yake ambayo iliyokuwepo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara na wawekezaji mbali mbali wanavutiwa sana kuekeza katika maeneo yale ya Mji Mkongwe kwa sababu ni maeneo ambayo yanatambulika duniani ni maeneo ambayo ya kibiashara.

Lakini tukija katika hoja yenyewe ilioko mezani suala la kubadilisha matumizi ya Skuli ya Darajani pamoja na Skuli ya Vikokotoni lakini kuivunja Skuli ya Vikokotoni ili iwe ni eneo moja kwa moja la kibiashara.

Maoni ya kamati yangu ambayo ni maoni ya kitaalamu. Mhe. Naibu Spika, maoni ya Kamati yangu ni kwamba suala la kuivunja Skuli ya Vikokotoni kamati yangu haikubaliani na wazo hilo na sio kwamba haikubaliani kwa sababu ya utashi, haikubaliani Mhe. Naibu Spika, kwa sababu Skuli ya Vikokotoni ni jengo ambalo lipo zaidi ya miaka 50 na kwa sheria na kwa taratibu za *UNESCO* jengo lolote ambalo liko zaidi ya miaka 50 hilo linatakiwa lilindwe ili katika kulinda ile *heritage* za Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu inashauri kwa upande wa Skuli ya Vikokotoni iendelee kubaki lakini inakubaliana na mawazo ya serikali kubadilisha matumizi ya Skuli ya Vikokotoni ili liwe ni eneo la kibiashara.

Kwa upande wa Skuli ya Darajani, kamati yangu haina matatizo kwamba skuli ile iendele kubaki. Lakini kuhusu matumizi ya skuli ile kamati yangu inakubali wanafunzi pale waondolewe ili wajengewe skuli nyengine ambayo itakuwa na mazingira mazuri ya kisasa.

Mhe. Naibu Spika, masharti ya *UNESCO* unapobadilisha matumizi ya eneo husika inabidi michoro ile ikishachorwa ipelekwe *UNESCO,* michoro ile ikipelekwa *UNESCO* itaangaliwa yale masharti halafu baadae watakuja kuulizwa wananchi husika wanaokaa katika maeneo yale. Sasa hofu ya kamati inapokuwa maoni ya wananchi wakija kuulizwa wanaoishi katika mazingira yale yakiwa na *negative impact* kwa kweli itakuwa mradi utachelewa kufanywa na mfanyabiashara au muekezaji ataendelea kuchelewa kutekeleza mradi wake.

Mhe. Naibu Spika, tuchukulie mfano wa Hoteli ya Bwawani. Hoteli ya Bwawani serikali imefanya mabadiliko ya matumizi eneo lile kwa mujibu wa maoni ya wataalamu walikubaliana kubadilisha matumzi kwa sababu jengo lile halijatimia miaka 50. Lakini kwa Skuli ya Darajani na Skuli ya Vikokotoni majengo haya yapo zaidi ya miaka 50 kamati yangu inashauri yalindwe.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia Mji Mkongwe faida zake urithi wa kimataifa umetusidia kuleta watalii wengi ambao wanaongeza mapato katika nchi yetu. Ukiangalia katika nchi nyengine Mhe. Naibu Spika, wewe mwenyewe shahidi. Mimi mwenyewe nikiwa pamoja na Mhe. Mnadhimu wetu wa CCM wa Baraza la Wawakilishi tumewahi kutembelea China na tulipotembelea China kuna maeneo ya historia mbali mbali ambayo yamehifadhiwa yamewekwa na watalii na wageni mbali mbali wanakwenda kutembezwa. Tumekuta kuna baadhi ya viwanda ambavyo tokea wakati wa Ukoloni vilipokuja kubadilishwa matumizi yake viwanda vile vimebakishwa pembeni vinajengwa viwanda vyengine pembeni.

Kwa hivyo, suala la uhifadhi kwa kweli ni suala muhimu, suala la kuvunjwa moja katika majengo yale kamati yangu kwa kweli haikubaliani. Lakini kubadilisha matumizi kwa maeneo yale Mhe. Naibu Spika, kamati inakubali kwa sababu eneo lile likiwa ni

*business centre* itakuwa ni zogo kubwa wanafunzi wetu watakuwa hawana raha ya kusoma.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, kamati yangu inaishauri serikali ni vizuri kubadilisha Ukanda wa *Darajani Corridor*, lakini ni busara zaidi kuanza kutumia hizo fedha ambazo serikali wamesema tayari wameshazipata kwa ajili ya kujenga skuli mpya za kisasa katika eneo la Rahaleo, ili wale wanafunzi watakaotoka skuli ya Darajani na Vikokotoni waweze kupata nafasi nzuri zaidi ya kuweza kusoma ili wapate kujiendeleza katika elimu yao ya baadae.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na naomba sana serikali yetu tujaribu sana kuwa wasikivu kusikiliza maoni ya wataalamu, lakini vile vile tuangalie namna gani ya kuweza kulinda historia yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya kamati nakushukuru sana, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Omar Seif Abeid, karibu.

**Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na kauli ya serikali, kuhusu uamuzi wa serikali wa kuivunja skuli ya Vikokotoni.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia kutukutanisha hapa leo. Lakini pia nachukua fursa hii kumpongeza sana Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi,

kwa kuwasilisha vyema kauli ya serikali kutokana na uamuzi wa serikali wa kuivunja skuli ya Vikokotoni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, maoni ya kamati yangu sisi baada ya kuipata taarifa hii, napenda kulieleza Baraza lako tukufu kwamba tulikaa tukatafakari na tukafikiria kwenye mambo matatu. Kwanza tulifikiria ni kwa nini serikali iliamua kuvunja ile skuli ya Vikokotoni. Lakini pia tukafikiria faida na hasara ambazo zingeweza kupatikana kwa kuvunjwa ile skuli ya Vikokotoni. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu tukafikiria yafuatayo. Kwanza tuliona uamuzi wa serikali ni uamuzi mzuri, ni uamuzi wenye busara, uamuzi wa hekima ambapo lengo la serikali ilikuwa na nia nzuri kwetu sisi raia wake, sio kwa maslahi yetu tu, lakini hata kwa maslahi ya vizazi vijavyo. Waliona kwa sasa serikali imefikia pahala pa kuiondoa ile skuli na wakaitafutia eneo mbadala kwa sababu mbili. *(Makofi)*

Kwanza jengo lenyewe la skuli limeshakuwa kongwe kama limeshakuwa kongwe ni vyema vijana wetu, kwa kulinda usalama wa vijana wetu lile jengo likabadilishwa. Kwa hivyo, tukalifikiria hivyo na tukalitafakari tukaona ni wazo zuri, sisi tumekubaliana nalo kwa sababu hiyo ya kwanza. Lakini pia kwa upande mwengine tukafikiria kama ni wazo zuri kwa nini tulijadili. Tukatoa mfano wa skuli ya Gulioni, skuli ya Gulioni ilikuwepo lakini kwa matumizi mazuri leo iko Benki Kuu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tukasema ni vizuri na ni busara tukatumia namna kama ile tukaondoa kitu kimoja tukaweka chengine, tukakubaliana kwamba kwa kuzingatia sababu hii ipo haja ya kuiondoa skuli ya Vikokotoni wakaitafutia eneo jengine liliopo karibu na mji, ili wanafunzi wetu watoto wetu wakapata kusoma vizuri, wakapata sehemu ya utulivu kulikoni pale Darajani.

Tukarudi Darajani sasa tukaitafakari Darajani ilivyo, tukasema Darajani ni sehemu iliyotengwa kwa ajili ya biashara, muingiliano wa wafanyabiashara ni mkubwa, watoto wetu hawapati nafasi ya utulivu. Kutokana na sababu hizi tatu kamati yangu ikaona ni vyema kuihimiza serikali na kwa sababu ina dhamira nzuri ifanye haraka kuliondoa jengo na ijenge jengo jengine mbadala ambalo litakuwa ni zuri zaidi ya lile kwa ajili ya wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa maoni ya kamati mimi ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, nachukua nafasi hii kutamka kwamba kamati yangu imeridhika na maamuzi ya serikali na tunaiomba serikali iweke jengo mbadala na iweze kuwahamisha wanafunzi walioko pale iwapeleke katika skuli hiyo nyengine. *(Makofi)*

Baada ya haya Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya kamati yangu na naunga mkono kauli ya serikali kwa asilimia mia. Ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Sasa nafikiri ni muda wa maswali, waliosimama wote wana nia ya kuuliza maswali nitawapa wajumbe watano kuuliza maswali. Naanza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Waheshimiwa Wajumbe, nawataja hawa kwa sababu wameleta majina yao mbele yangu, kwa hivyo ndio maana nawataja. Baada ya hapo atafuata Mhe. Nassor Salim Ali na baadae atakuja Mhe. Simai Mohammed Said, na nitampa nafasi Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, halafu nitampatia na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na wa mwisho kabisa atafuata Mhe. Ali Salum Haji. Nafikiri nimewamaliza. Tunaanza na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Karibu sana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kuweza kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza

zito hili chombo cha kutunga sheria. Mhe. Naibu Spika, nchi yetu inaongozwa na Katiba ya Zanzibar, hata hili Baraza lako linaongozwa na kanuni na nchi yetu inazungumzwa...

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, ni swali sio mchango nimesema, ni maswali sio mchango, naomba uelekeze swali moja kwa moja kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ni swali sio mchango.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ndio nakuja huko Mhe. Naibu Spika, kujenga hoja, maana yake tunaongozwa na katiba ya 43(5), Baraza la Mapinduzi kifungu 5 cha sheria namba 11(9)(5), kifungu cha 27 cha sheria namba 9 ya 2000.

a) Kutakuwa na Baraza la Mapinduzi ambalo litajumuisha Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais, Mawaziri pamoja na wajumbe wengine, kama Rais atakavyoona inafaa.

b) Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi watateuliwa na Rais kutokana na miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

c) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atahudhuria mikutano yote ya Baraza la Mapinduzi na atakuwa na haki zote kama mjumbe.

Mhe. Naibu Spika, kazi za Baraza la Mapinduzi zitakuwa;

a) Kumsaidia na kumshauri Rais katika masuala ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;

b) Kuratibu

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Jaku Hashim  Ayoub hayo maelezo yote ya nini, nimesema nenda kwenye swali lako unalotaka kuuliza, hayo yote yanafahamika. Nenda kwenye swali mheshimiwa.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Hoja yangu hapa serikali nafikiri haikuwa tayari kwa ushahidi huu niliokuwa nao.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji**: Katika swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub yeye aliuliza na alizungumzia suala la kwamba haafiki wazo la kuzivunja skuli za Darajani na Vikokotoni na kumshauri Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mkongwe kuishauri serikali kuhusu suala hilo.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kumjibu mheshimiwa kwamba wizara imelipokea hilo na kulifikiria kutokuzivunja skuli kutokana na malalamiko ya wananchi katika serikali jambo hili limetokana na kusema.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Sasa Mhe. Naibu Spika, huku kuna kauli nyengine na huku kuna kauli nyengine. Ndio nikasema haya maamuzi serikali bado haijawa tayari, hawa wanawajibika kwa pamoja, humu tunaiuliza serikali hatumuulizi waziri, kuna kauli mbili hizi na haya sio maneno yangu ni *hansard* na vyombo vya habari vimetangaza.

Kwa hivyo, mimi naishauri serikali warudi wakajipange tena kuhusu suala hili, haijawa tayari, haya sio maneno yangu, ndio nikasema taratibu hizi. Kwa hivyo, wakajipange.

**Mhe. Naibu Spika:** Sawa. Maliza swali lako Mhe. Jaku Hashim Ayoub, malizia.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, hoja yangu ndio hii hapa kuna kauli mbili, na humu tunavyouliza tunauliza serikali

hatumuulizi waziri, wanafanyakazi kwa kumshauri Mhe. Rais. Kwa hivyo, wakajipange warudi tena na hili swali, tuliondoshe leo hili kutokana na kauli hii. Naomba nikuletee uione hii, hili suala tulirudishe ili ikajipange. *(Hebu shika mpelekee Naibu Spika hii).*

**Mhe. Naibu Spika:** Haya, wamesikia serikali itakujibu, wameshakusikia. Ahsante Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Muulizaji wa pili wa swali ni Mhe. Nassor Salim Ali.

**Mhe. Nassor Salim Ali:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi ya kuuliza swali. Mhe. Naibu Spika, katika ripoti hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inasema kwamba wanafunzi wanaosoma katika skuli hizo watajengewa skuli mpya ya kisasa katika eneo la Rahaleo ambapo fedha za ujenzi wake zimeshapatikana kwa kupitia mfuko wa *OPEC*.

Mhe. Naibu Spika, swali langu ni kwamba katika eneo la Rahaleo ambapo mimi ndio Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni na nimo katika maeneo hayo ya Rahaleo, kuna skuli ya msingi ya Rahaleo, lakini vile vile kuna skuli ya msingi ya Mwembeshauri. Swali langu ni kwamba je, ujenzi huu utajengwa katika skuli ya msingi Rahaleo au utajengwa katika skuli ya msingi Mwembeshauri ambayo tayari ujenzi wa skuli ya Mwembeshauri uko katika mpango wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Je, ni eneo gani skuli hii mpya itajengwa ambayo ni ya kisasa.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Mhe. Naibu Spika, swali langu mimi ni dogo kabisa. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa eneo la Mji Mkongwe pamoja na hiyo…

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, minong'ono imezidi naomba tuwasikilize wale ambao wanauliza maswali. Mhe. Mjumbe endelea.

**Mhe. Simai Mohammed Said:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa eneo la Mji Mkongwe pamoja na eneo hilo ambalo ni la *Stone Town Greater* Mji Mkongwe ambayo ni Vikokotoni, Darajani na maeneo mengine, pia yamo yanatambulikana kwa njia moja ndani ya urithi wa dunia.

Lakini moja katika *component* ya urithi wa dunia na katika kuitumia *heritage* kuibadilisha pia katika eneo moja kukuza uchumi, au nasema kutumia *heritage* pia ilete manufaa kwa nchi kwa maslahi ya kuweza kusaidia au kujikwamua au kuongeza pato kwa kujenga uchumi wako. Swali langu liko hivi.

Mhe. Naibu Spika, katika mawazo au fikra ambazo zimekuja ndani ya serikali ni moja ya ahadi hivi sasa tumesikia ni kuli-*transfer* eneo hilo au kuzivunja eneo moja la hizo skuli kwa kujenga eneo la aidha *shopping mall* au mawazo hayo. Nataka kufahamu je, ni wawekezaji wangapi ambao tayari serikali imewafikiria au kuna mpango wa kutoa tenda juu ya suala zima. Lakini pia je, katika mpango huo ni aina gani ya wawekezaji ambao tayari serikali imefikiria ambayo itaendana sambamba na mazingira ya Mji Mkongwe, ili kuhakikisha kwamba huo urithi wetu tunazidi kuulinda kwa manufaa ya vizazi vyetu vinavyokuja, ahsante sana.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante. Anayefuata ni Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

**Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *Bismillah Rahman Rahiym,* nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nilikuwa sitaki kabisa kuchangia, lakini kwa mambo haya ambayo yamejitokeza kwamba kuna vitu vinakuwa sio vizuri nimeamua na mimi kuuliza maswali.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma alipokuja hapa na maoni ya kamati yake, alieleza ukumbi ambayo kayafanyia

uchunguzi na akatizama pande zote mbili, moja za kibiashara na za ki-*heritage* kwa maana mambo ya kiasili. Lakini kamati iliyokuja nataka ije itujibu itueleze, wamefuata vigezo vipi au wamefuata ushauri gani, maana yake kwenye *heritage* hajaingia kabisa kataja kwengine tu. Kama kamati wameshirikiana vipi na upande wa *heritage* kuangalia faida na hasara za mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, swali langu jengine ni kwamba, sawa skuli ipo kwenye sehemu ya zogo na ndio maana inataka kuhamishwa. Lakini tunafahamu kwamba sehemu nyingi kuna shule kama hizo ambazo ziko sehemu ya zogo zinatiwa *sound proof.* Kwa nini serikali isifikirie kutia vioo vya *sound proof* ili wanafunzi wasome vizuri bila ya zogo kusikilikana.

Mhe. Naibu Spika, swali jengine tumeona kwamba sehemu nyingi serikali inazuia na bado hazijajengwa, likiwemo jumba la treni na kutokana na hivyo hivyo masuala ya vibali. Kwa hivyo, ningeomba kujua je, wameshapewa barua ya *UNESCO* kwamba iko *under heritage* skuli ya Darajani. Wameshapewa barua ya *UNESCO* kukubaliwa kufanya hivyo wanavyotaka wao.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante. Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwanza naomba kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita nafikiri kwa kuweza kuja na wazo la kusahau au ku-*forget about world heritage* na kuwapa pale Hyatt kujengwa.

Mhe. Naibu Spika, sote ni mashahidi kabla ya kujengwa ile hoteli ya Hyatt pale pahali palikuwa pabovu na panavunja moyo, leo ni pazuri kwa kusahau *world heritage*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka kuuliza swali, hivi kama Mjerumani, Muingereza na Mmarekani wanataka kuleta

maendeleo katika eneo lao kujenga, *would they consider the world heritage? The answer is no. (Makofi)*

Sasa Mhe. Naibu Spika, tunataka kujenga *shopping mall* tunahitaji eneo kubwa, tunataka ku- *consider parking space*, tunataka ku-*consider environment green*, tunataka ku-*consider* mambo mengi katika kujenga *shopping mall* ambayo iwe *sustainable*, kizazi cha leo na kizazi cha kesho kisije kikatutukana kwamba hawa jamaa walijenga nini.

Mhe. Naibu Spika, katika kufanya hivyo katika ulimwengu ulioendelea, *we have to consider* vitu vyote hivyo. Mhe. Naibu Spika, kwa nini serikali isizibomoe skuli zote za Vikokotoni na Darajani, ili tukapata nafasi ya kuvijenga vitu hivyo. Kama si hivyo Mhe. Naibu Spika, maoni yangu mimi na mawazo yangu mimi pale pahala hapafai ni padogo. Kama serikali inaangalia kutobomoa skuli zote mbili na kubomoa moja. *(Makofi)*

Swali langu, kwa nini serikali haioni sababu isiende ikaangalia eneo jengine kwa mfano Tunguu na pahala pengine kwa kujenga kitu hicho, kwa sababu eneo lile litakuwa dogo na halitoshi. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Hassan Khamis Hafidhkwa swali lako. Mhe. Ali Salum Haji, baadae atafuata Mhe. Hussein Ibarahim Makungu.

**Mhe. Ali Salum Haji:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, mimi kabla sijauliza swali langu niipongeze serikali kwa maamuzi mazuri ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. Kabla sijauliza swali na mimi niipongeze serikali kwa maamuzi mazuri ya kubadilisha mji wetu na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Maswali yangu mimi ni madogo tu. *(Makofi)*

Moja, kutokana na kubadilisha matumizi ya Skuli ya Darajani serikali imejipanga vipi kuweka historia baada ya kubadilisha matumizi ili vizazi vinavyokuja vielewe kwamba pale kabla ya matumizi ya mambo ya kibiashara ilikuwa ni skuli ya Darajani. Maana yake watatunza vipi kumbukumbu za historia ya skuli ile.

Pili, kutokana na kubadilisha mazingira ya kibiashara badala ya skuli nilitaka kujua mabadiliko ya jengo lenyewe ya ndani yatabadilika kwa asilimia ngapi, ili tusije tukaondosha mazingira na haiba ya Mji Mkongwe.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante swali la mwisho anayetaka kuuliza swali.

**Mhe. Ali Khamis Bakar:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali. Kwanza na mimi niipongeze serikali kwa maamuzi mazuri ambayo iliyafanya na kutuwasilishia mbele yetu, najua walishafikiria sana ndio maana wakaona ipo haja ya kubadilisha katika hilo eneo ambalo walilikusudia.

Mhe. Naibu Spika, mimi swali langu lipo hapa. Je, hao wanafunzi ambao wanaondoshwa na kuwekwa katika skuli nyengine, hii skuli kwanza itajengwa mwanzo ndio baadae wao waambiwe wabakie katika hiyo skuli ambayo itajengwa, ama kutafanywa uvunjaji kwanza kama vile ambavyo tumeona baadhi ya maeneo mengine ambayo sasa hivi yako wazi na ndio baadae wale wanafunzi wahangaike. Mimi nilikuwa nataka kujua je, kwanza hawa wanafunzi watatafutiwa sehemu nzuri ya kutulizana, yaani skuli nyengine ambayo imekusudiwa kujengwa wapate maeneo ya kukaa kwanza ndio baadae uendelee huu uvunjaji ama vipi.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa nawashukuru wale wote ambao wameuliza maswali, sasa nafikiri ni wakati wa serikali kujibu maswali hayo. Nitaanza na Mhe. Haji Omar Kheri na

baada ya hapo atafuata Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, na baadae tutampisha mwenye hoja Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Haji Omar Kheri karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kutoa ufafanuzi juu ya mchango wa Kamati na kutoa ufafanuzi juu ya baadhi ya maswali ambayo yamejitokeza. Kwanza nianze na mchango wa Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ujenzi na Mawasiliano, Mhe. Hamza Hassan Juma.
Kwanza nataka nilithibitishie Baraza lako tukufu la Wawakilishi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipofanya maamuzi ya kuliendeleza eneo la Ukanda wa Darajani iliwatumia wataalam wake wote wanaohusiana na suala la Mji Mkongwe, wanaohusiana na masuala ya Mazingira, wanaohusiana na masuala ya Mipango Miji na Vijiji pamoja na ma-*engineer* na wataalam wanaotokea Baraza la Manispaa Zanzibar. Kwa hivyo, lile alilolizungumza Mhe. Hamza Hassan Juma la kwamba wataalam wameishauri serikali au amefanya utafiti kwa wataalam na pengine hawakushauriwa au hawakushirikishwa, watalaam hawa ndio waliotushauri kwa historia kama ifuatavyo.

Kwanza, Skuli ya Darajani ingestahiki kubakia na ikabadilishwa matumizi ikatengenezwa mle ndani ikawepo biashara zinazohusiana na asili ya kizanzibari kwa sababu ya historia yake kama alivyolizungumza Mheshimiwa mmoja hapa kumbukumbu zitakuwaje. Kumbukumbu kuna za namna mbili, kuna kumbukumbu kwa maana ya kubakisha jengo, jengo litabakia lakini kuna kumbukumbu kwa maana ya maandishi, maandishi yatakuwepo kwenye jengo lile na kuonesha kwamba skuli hii kumbukumbu zake na historia yake ni hii. Kwa hivyo, kumbukumbu za maandishi zitakuwepo na kumbukumbu za jengo zitakuwepo hakuna tatizo kuhusu wale wajumbe ambao wameuliza maswali ya kumbukumbu.

Wataalam wa Mji Mkongwe, wataalam wa Mipango Miji, wataalam wa Mazingira, wataalam wa Manispaa na ma-*engineer* wengine ndio walioishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuivunja Skuli ya Vikokotoni na kujenga *Shopping Mall.* Mhe. Hamza Hassan Juma alisema vizuri sana kwamba skuli hii ina umri wa miaka 50. Kwa nini Skuli ya Vikokotoni ilijengwa? Ilijengwa Skuli ya Vikokotoni baada ya serikali ya wakati huo kuivunja skuli ya Shimoni kwa kuJenga Uwanja wa Mao-Tse-Tung, ilikuwepo skuli lakini kwa sababu ya haja ya wakati ule na maendeleo ya kuwepo *Stadium* skuli ya Shimoni Kikwajuni ikavunjwa *replacement* ikenda ikafanywa Vikokotoni. Kwa mnasaba huo huo, kwa sababu ya *development* kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar na maslahi ya Zanzibar, ndio maana Serikali inaamua kuivunja skuli ya Vikokotoni kujenga *Shopping Mall*.

Kwa hivyo, historia tunaikubali lakini na *development* tunaihitaji Zanzibar nataka nimtoe wasiwasi Mhe. Hamza Hassan Juma kwamba wataalam hawa wanaotushauri ndio wataalam wa Zanzibar, wataalam wa Mazingira kama nilivyosema mwanzo, wataalama wa Mipango Miji, wataalam wa Manispaa na hatimae tutazingatia taratibu na kanuni tulizojiwekea sisi wenyewe na sheria tulizoziunda zinazohusiana na suala la uhifadhi wa Mji Mkongwe. Serikali tunafanya hivyo kwa uangalifu mkubwa sana.

Jengine ambalo nataka niliseme ni swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwanza sekta inayosimamia jambo hili ni Sekta ya Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Mhe. Jaku na wengine swali hili hili kwenye mjadala wa bajeti ya ofisi yangu liliulizwa na nilitoa ufafanuzi, kama *hansard* ilikuwa achukue *hansard* zote mbili iliyozungumzwa na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji na iliyozungumzwa na Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Ndio maana Mhe. Waziri wa Ujenzi akasema

tutakwenda kushauriana kwa kifungu kile kile cha katiba alichokisoma Mhe. Jaku kinachowafanya Mawaziri wawajibike kwa pamoja baada ya kushauriana, ndio maana serikali kupitia Makamu wa Pili wa Rais imekuja na kauli na maamuzi ya awali ya serikali.
Kwa mujibu wa kifungu cha 43(5) cha Katiba ya Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi ya sera za serikali kwa jumla na Mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili wa Rais watawajibika kwa pamoja katika Baraza la Wawakilishi kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, haya ndio maamuzi ya serikali ambayo kikatiba ndio imepewa mamlaka ya sera kuweka sera na mipango ya nchi na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inatuelekeza tufanye hayo. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi nilisema nitoe ufafanuzi juu ya maeneo hayo machache kwamba serikali iliamua na ndio maana waziri alisema atakwenda kushauriana. Kwa hivyo, serikali tumeshauriana tumerudi na maamuzi ya serikali ambapo tunawajibika kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono kauli ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**Mhe. Naibu Spika**: Ahsante sana Mhe. Haji Omar Kheri sitaki sasa hivi utaratibu naomba ukae Mheshimiwa hapa hatuna nafasi ya utaratibu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Baraza linapotoshwa sio.

**Mhe. Naibu Spika:** Hapana hapana naomba ukae tuendelee na shughuli. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, lakini pia nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kutoa kauli hii ya serikali ambayo ina umuhimu wake na historia yake katika siku ya leo. Aidha, nimpongeze na kumshukuru sana Mhe. Balozi Ali Abeid Karume kwa busara zake wakati alipokuwa anajibu hoja katika wizara yake alieleza wazi kwamba jambo hili angelichukua na kwenda kushauriana na serikali ili lije jibu muafaka na leo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ameleta jibu kwa niaba ya serikali. Kwa hivyo napenda sana nimpongeze Waziri Balozi Ali Abeid Karume. *(Makofi)*

Aidha, nimpongeze Mhe. Haji Omar Kheri kwa kueleza kwa ufasaha msimamo wa serikali katika jambo hili. Mimi nirudie kusema Mhe. Naibu Spika, kwamba dhamira ya serikali ni kulinda urithi wa kimataifa wa Mji Mkongwe hilo halina mjadala wala hatuna katika serikali kauli zinazopingana, tuna kauli moja ambayo tunaafikiana. Tunafanya hivyo kwa sababu tunashauriana na hatushauriani kwa maslahi ya mtu mmoja mmoja tunashauriana kwa maslahi ya taifa na wananchi wa Zanzibar kwa jumla. Kwa hivyo, maamuzi yanayofanywa yana misingi ya kulinda uhai wa taifa letu, kulinda uhai wa wananchi wetu na kujenga mazingira mazuri kwa vizazi vinavyokuja katika nchi yetu. Kwa hivyo uamuzi ule ulilenga kuimarisha uasili wa eneo la Darajani.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya hapo Darajani kilikuwa ni kitovu kikuu cha biashara kwa Zanzibar na ikaendelea hivyo mpaka leo. Kabla ya skuli zenyewe kilikuwa kitovu cha biashara na kwa sababu ya dunia ya leo na umuhimu wa kuimarisha biashara na uchumi kwa nchi yetu na kuendeleza uasili wake ndio serikali imefanya maamuzi yale. Kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, maamuzi yale yalifanywa baada ya tathmini ya kina iliyowahusisha wataalam wetu wote wa kimazingira, wa Mji

Mkongwe, wataalam wa uchumi, wataalam wa biashara na wananchi kwa jumla katika kupata uhalisia wa maeneo yake. Pia tukumbuke kwamba eneo lile wanafunzi wetu walikuwa wakinyanyasika sana kutokana na shughuli za biashara zinazofanywa pale, lakini na baadhi ya waliofanya shughuli zile pale na wasiokuwa wanafanya pale lakini wakija pale walikuwa wanawasumbua wanafunzi wetu wanafanya mambo kinyume na silka na utamaduni wa kizanzibari.

Kwa hivyo, hatua za makusudi katika kuondoa hayo na katika kuhakikisha wanafunzi wetu wanasoma kwa utulivu na kulinda historia yetu ndio maana uamuzi ule ukafanywa ili tuendelee na kuwa na mji wenye haiba, wenye kuvutia, unaopendwa na wengi. Tunapovunja Skuli ya Vikokotoni kama tulivyosema na iwe ni jibu kabisa la baadhi ya Wajumbe walioiuliza ni kwamba tunajenga skuli katika eneo la Rahaleo *primary* ya kisasa itakayoweza kuchukua wanafunzi waliopo na kuchukua na wanafunzi wote wa Darajani na Vikokotoni. Katika tathmini iliyofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wanafunzi wote hao katika eneo la Rahaleo inakuwa ni karibu yao zaidi. Kwa msingi huo, wanafunzi watakuwa hawapati usumbufu wanapokwenda hapo na skuli hiyo itajengwa kabla ya kuvunjwa au kabla ya kufanyiwa matengenezo skuli zile ambazo zitataka kufanyiwa marekebisho. Taratibu zote zinafuatwa tunayo sheria yetu Nam. 4 ya mwaka 2010 inayozingatia taratibu za Mji Mkongwe, taratibu hizo zimefuatwa na mapendekezo yetu ya namna ya ujenzi wa eneo la Darajani yamewasilishwa *UNESCO* kwa maoni yao na pale itakapokamilika watatoa maoni yao na baada ya hapo ujenzi utaanza na utaratibu rasmi wa ujenzi huo utatangazwa na mwenye kuwa na hamu na nia ya kushiriki atakaribishwa.

Lakini serikali yenyewe imepanga mipango yake vizuri ya namna ya kuliimarisha eneo lile ili liwe la kisasa, liwe la kibiashara, liwe la kuvutia. Nataka nikuhakikishieni Waheshimiwa Wajumbe

kinachofanyika kina maslahi makubwa na nchi yetu, kina maslahi makubwa na vizazi vyetu vya leo na vizazi vinavyokuja. Kwa hivyo, mambo yote muhimu yanayozingatia utaratibu wa urithi wa Mji Mkongwe yamezingatiwa na yote yatafuatwa ili kuendeza kuimarisha dhana ya Mji wetu Mkongwe, ni sisi wenyewe Zanzibar tulioamua kuuhifadhi mji huo. Mtu yeyote yule au nchi yeyote ikiwa Uingereza, ikiwa Ujerumani ikiingia katika makubalino ya uhifadhi wa Mji Mkongwe inafuata taratibu kama ambavyo sisi tunazifuata. Tunaamini sana kwamba tutapata mashirikiano mazuri na wenzetu wa *UNESCO* wakati wa kuendeleza eneo letu hilo.

Naamini kwa jambo lolote jema na jambo la kimaendeleo tunaweza kupata malalamiko ya hapa na pale lakini shughuli itakapomalizika naamini sana Wajumbe wote wale watatupongeza na watasema serikali imeamua kitengo kizuri na cha maana na maendeleo ya nchi yetu. Kwa hivyo, naamini sana Mhe. Naibu Spika, kama alivyokwishasema Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwamba kumbukumbu za eneo zile zitakuwepo, maandishi yatakuwepo, kwa hivyo hakuna jambo ambalo litabadilika isipokuwa tutazidi kujenga jambo ambalo litakuwa na maendeleo makubwa zaidi ya kiuchumi na kibiashara na kuhifadhi uasilia na utamaduni wetu wa Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga tena mkono kwa asilimia mia moja kauli ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ambayo ni Kauli ya Serikali kwa ajili ya kuendeleza mji wetu hasa katika kuendeleza eneo la *Darajani Corridor*. Ahsante sana nakushukuru.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Sasa naam!

## UTARATIBU

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza utaratibu. Labda kabla ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hajaja kutoa majumuisho nilitaka nijue swali moja tu. Sasa hivi tumetangaza eneo la Kijangwani kuwa ni *stand* kuu ya daladala na skuli hizi zinazohamishiwa huko zitahamia pale skuli ya Rahaleo. Hatuoni kwamba bado yale mazingira ya zogo tuliyoyakimbia huku na pale bado yataendelea kuwepo. Ahsante. *(Makofi)*

**Mhe. Naibu Spika:** Mheshimiwa umeuliza swali lakini serikali nayo iko tayari kulijibu vile vile. Sasa nimwachie Mhe. Haji Omar Kheri anaweza kulijibu swali hilo kabla ya kumpisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Haji Omar Kheri karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa swali ambalo ameliuliza Mhe. Hamza Hassan Juma na hapa nataka nitumie nafasi ya kujibu swali moja ambalo hatukulijibu alilouliza Mhe. Hassan linalohusiana kama eneo la Darajani ni dogo kwa nini tusiende katika maeneo mengine. Eneo la Darajani ni sehemu ya mji ambalo linajumuisha maeneo ya karibu ya makaazi ya watu, kwa hiyo serikali imeona pale lazima pawe na *Business Centre*. *Business Centre* ambayo itawasaidia watu wanaoishi katika maeneo ya karibu na watu watakaokuja kutembelea katika maeneo yale.

Pale niliposema jambo hili linazingatia pia mpango mkuu wa *Master Plan* ni kwamba ni katika maeneo tofauti kila pahala pamewekwa huduma kama hizi za kijamii na kibiashara. Kwa hiyo, huko ambako Mhe. Hassan alisema Tunguu kutakuwa na mipango hiyo, Fumba kutakuwa na mipango hiyo, Mazizini kutakuwa na mipango hiyo, Michenzani kuna mipango hiyo na miji mingine mingi ambayo serikali imeona ianzishwe kutakuwa na huduma kama hizo.

Kuhusu suala la Mhe. Hamza Hassan Juma serikali inataka kuhamishia kituo cha daladala au *stand* katika eneo la Ng'ambu kwa maana ya kati ya Rahaleo, Mwembeladu na Kijangwani. Tutakumbuka kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha *Master Plan* ambayo ndio iliyotoa matokeo ya kuwepo kwa jengo la *BoT*, jengo la Shirika la Umeme na majengo mengine. Posta kwa hivi sasa kuna jengo la Shirika la Umeme, jengo la Posta na jengo la *BoT*. Lakini katika *line* ile yote mpaka unafika Kilimani itakuwa ni sehemu ya *Business Centre* na majengo ya ofisi na huduma za jamii.

Kwa hiyo katika mipango miji ipo shule, kipo kituo cha daladala, mpango uliopo utatofautisha kabisa eneo la shule na eneo la daladala  na unaweza ukajiuliza, sasa hicho kituo cha daladala kitakuwa wapi. Serikali ikishakupanga kama tunavyofanya katika eneo la Vikokotoni na eneo la Rahaleo tutafanya vile vile, kuna majengo itabidi yaondoke ili yaje yale majengo yatakayotoa huduma kwa jamii. Kwa hiyo, shule imepangwa ijengwe mkono wa kushoto kama unakwenda Kinazini au unakwenda Mwembeladu, ijengwe shule ya ghorofa ambayo itakuwa ni shule bora, shule kubwa itakayokidhi mahitaji ya wanafunzi wanaosoma katika skuli ya Darajani na Vikokotoni na wanafunzi wengine wanaosoma ng'ambu.

Kwa hiyo, serikali imelizingatia hilo na kutakuwa na tofauti kati ya eneo la kituo cha daladala na eneo la skuli inapojengwa. Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa majibu yako mazuri kabisa, sasa nimpe nafasi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aje kwa ajili ya kujibu maswali. *(Makofi)*

**Mhe. Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii tena ya kuja kujumuisha

mambo yote yaliyozungumza na kuulizwa na Wajumbe wa Baraza.

Mhe. Naibu Spika, tunataka kujenga mji wetu uje uwe mzuri, uwe wa haiba, uwe wa kuvutia na sehemu yoyote ile ambayo unataka kujenga mji mzuri, lazima kubomoa sehemu fulani na ukajenga majengo mapya. Mhe. Hamza Hassan Juma amezungumza China Mhe. Naibu Spika, mimi nimekaa China miaka tisa na maendeleo ya pale nimeanza kuyaona toka mwaka 1978 nimekwenda China kabla hawajapata maendeleo ya sasa na mpaka wamepata maendeleo ya sasa. Kwa mara ya mwisho nimeondoka China mwaka 1998, kwa hivyo walikuwa na majengo pale ya kizamani lakini kwa sababu ya kuleta haiba ya mji wao majengo yale yamebomolewa yamejengwa majengo mapya ya kuvutia ya ghorofa. *(Makofi)*

Sasa leo ukenda China kila mmoja anasema, China bwana imeendelea, lakini imeendelea vipi havikuachwa vile vituturi vikaweko pale mjini vimebomolewa yakajengwa majengo mapya ndio mji mpya leo wa China tunavyouona. Lakini hata Dar es Salaam leo tunakwenda tuna-*admire* Dar es Salaam nzuri inaendelea, lakini majengo ya zamani yapo sio yamebomolewa yakajengwa mengine mapya mazuri ndio maendeleo tunayoyataka. Nasema "tukiona vinaelea vimeundwa" na sisi tunataka kuunda. Kwa hivyo, mimi niwashukuru sana wale waliotoa michango yao Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano na Mwenyekiti wa Kamati ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa michango yao mizuri, lakini pia niwashukuru sana wale walioiliza maswali ambao naamini kabisa kwa maswali, mchango wa Mhe. Waziri wa wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kayajibu vizuri katoa ufafanuzi mzuri, naamini kabisa kwamba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu wameridhika. *(Makofi)*

Pia ule mchango uliotolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais nao umetoa ufafanuzi mzuri, umejibu maswali na naamini kabisa kwamba michango yao hiyo imetoa ufafanuzi wa kutosha. Dhamira yetu ni kujenga mji wetu na sisi watu waje ku-*admire* mji wetu kuwa mzuri. Hivi sasa si ndani ya Baraza hili wala sio ndani ya vikao vya Chama wananchi walikuwa wakilalamika hali iliyoko Darajani namna gani wanafunzi wetu walivyokuwa wanadhalilishwa pale na wafanyabiashara ndogo ndogo. Leo tunaziondoa skuli hizo kupisha ujenzi *mall* mfano tunaziacha hizo skuli ziendelee na shughuli zake za kiskuli, yanajengwa majengo ya *shopping mall* mkusanyiko wa watu utakuwa mkubwa ndani na nje ya nchi hali itakuwaje, patakuwa vurugu wanafunzi wetu hawatapata utulivu wa kusoma. *(Makofi)*

Ndio maana Serikali ikaamua kubomoa Skuli ya Vikokotoni ili ipatikane nafasi ya kutosha kujenga *shopping mall* na Skuli ya Darajani kuibadilisha ili iendane na shughuli za kibiashara zinazokuwepo pale Darajani. Kwa hivyo, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakubaliane na maamuzi ya Serikali kila mmoja wetu anataka mji wetu usifiwe kwa uzuri na haiba, hatutaki tuishi katika karne zile zile za miaka iliyopita, karne ya 21 lazima sisi Zanzibar tubadilike.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba tena wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakubaliane kabisa na maamuzi haya ya Serikali. Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, napenda niwatambue waliochangia kauli hii nianze na:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Omar Seif Abeid
3. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
4. Mhe. Nassor Salim Ali
5. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
6. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
7. Mhe. Simai Mohammed Said

8. Mhe. Ali Salum Haji
9. Mhe. Haji Omar Kheri na
10. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed

Nawashukuru sana kwa michango na ufafanuzi waliotoa.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa kauli.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nitaomba tu na mimi nisimame kidogo niipongeze sana Serikali kwanza kwa kuleta taarifa hii muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu, lakini niwapongeze na Waheshimiwa Wenyeviti kwa kutoa *concern* zao kuhusiana na suala hili kwani nafikiria kwamba ni moja ya kazi zetu za Wawakilishi. Lakini naomba sana waiamini Serikali kwenye hili lazima twende mbele hatuwezi kusimama. Historia itabaki pale pale na majengo yale yanaonesha historia hata ile historia ambayo tunasema ni ya kuzungumzwa baina ya watu. Kuna historia nyingi unaweza kuweka *documentation* lakini kuna historia ambayo inaendelea kwa sababu kuna watu wameipitia historia ile kwa hivyo itabakia pale pale.

Lakini tuseme tu kwamba juzi imekuwa nchi ya Namibia wamepiga hatua sana katika masuala ya maendeleo ya majengo na wamevunja wametoa baadhi ya maeneo ambayo wamehisi kwamba kunaweza yakaja mengine yatakayokuwa yana umuhimu zaidi. Kwa hivyo, tukubali lazima tusonge mbele Waheshimiwa wengi mmesafiri mmekwenda nje mmeona wenzetu namna walivyoendelea, namna miji yao ilivyobadilika hata huko tunasema kwamba nchi zilizoendelea wameondoa maeneo makubwa sana ambayo yana historia lakini kwa sababu ya maendeleo ya wananchi wake.

Kwa hivyo, naipongeza sana Serikali na nafikiri wengi wetu tuna hamu kubwa ya kuona hayo mabadiliko ya Mji Mkongwe wa

Zanzibar. Tutabakia kuwa tunadumisha historia yetu, lakini lazima tujue kwamba itafika wakati Waheshimiwa tunataka kupata mabadiliko. Tunapongeza sana Serikali sasa nafikiria Waheshimiwa Wajumbe kwamba tuendelee na utaratibu wetu mwengine ambao ni wa Waziri wa Fedha na Mipango. Lakini kabla ya hapo Waheshimiwa nitawaita wachangiaji wawili, nitamwita Mhe. Rashid Ali Juma na baadae Mhe. Jaku Hashim Ayoub ameniomba dakika tano.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka 2017/2018

*(Majadiliano yanaendelea)*

**Mhe. Naibu Spika:** Kanuni zetu hazina ulazima wa taarifa ya Serikali kupigiwa kura au kwamba kutoa hoja, hoja ile tayari imeshaletwa na Serikali kwa hiyo kanuni zetu ziko wazi kwamba ile hoja tumeipokea kama kawaida na tayari kwamba tumeshaipokea ndio maana tunaendelea. Sasa nakuomba sana Mhe. Rashid Ali Juma muda umekwenda kwa hivyo tutumie muda mdogo katika hoja hiyo ambayo unataka kuchangia na baadae nitampisha Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwa dakida tano tu. Karibu Mheshimiwa.

**Mhe. Rashid Ali Juma:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na kunipa fursa hii sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu na yeye kuweza kujaalia kwa asubuhi hii ya leo na mimi kupata fursa kuweza kuwawakilisha, hususan wananchi walionichagua wa Jimbo la Amani na mimi kupata kutoa mawazo yao ili kuweza kuchangia hii Hotuba ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Lakini pia nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kudhihirisha ule ushindi wake wa asilimia 94.1 alioupata na jinsi gani anavyoweza kusimamia majukumu yake katika ilani ya chama chetu, ili kuhahikisha kwamba maendeleo kupitia Sekta ya Fedha yanapatikana tena kwa wakati na muda muafaka. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nisiwe na mengi sana lakini nilikuwa nataka kuchangia ili niweze kwenye hoja ambazo zilichangiwa na baadhi ya wajumbe wetu kwa kuweka hofu baadhi ya maeneo walikuwa wakiyachangia na kuwapelekea kuweka hata asilimia 99.9 ya kukubali hotuba iliyotolewa na kubakisha asilimia ndogo sana mpaka pale ambapo watatolewa hofu juu ya hayo. Hivyo, kwa mtindo kama huu wa kufanya kazi za Serikali kwa pamoja nimeona niyachangie baadhi ya maeneo hayo, naamini wazi kwamba Wizara ya Fedha na Mipango iko bega kwa bega kushirikiana na taasisi nyengine zilizo karibu. Lakini vile vile na Wizara zote ambazo zimo katika Serikali yetu ikiwa pamoja na kufanya kazi pamoja *private sector* ikijumuishwa na mashirika ambayo yanajitegemea.

Mhe. Naibu Spika, jitihada za Wizara ya Fedha zinazofanywa katika Serikali hii zinaonekana wazi, kuanzia ile miaka 1990 ambayo wengi tumekuwa mashahidi hapa. Mhe. Naibu Spika, ilipofika miaka ya 1990 tulijua wazi kwamba zao letu la karafuu ambalo lilikuwa ni mhimili mkuu wa kutegemea uchumi lilianza kudorora na uchumi wetu ulianza kuja chini kwa kutegemea lile zao moja. Lakini cha kupendezesha zaidi kupitia Wizara hii ya Fedha ndani ya miaka ya 90 ilishauriana vizuri pamoja na Serikali yetu na kuanzisha njia mbadala ya kuanzisha utalii mnamo mwaka 1991-1992, utalii ukashika kasi ili Serikali iwe na njia mbadala ya kuweza kupata mapato na kuweza kuendeleza uchumi wake katika kuwahudumia wananchi. Jambo hili ni la faraja kuona hivi sasa katika miaka ya 2000 tunayokwenda nayo tayari Serikali yetu inategemea sana sekta ya utalii ambayo inachangia

zaidi asilimia 27 ya Pato la Taifa. Lakini vile vile inachangia zaidi asilimia 80 ya fedha za kigeni.

Mhe. Naibu Spika, jitihada zinazoonekana katika Wizara ya Fedha ziliendelezwa mnamo mwaka 1994-1996 wakati ilipoanzisha Kitengo cha Ukusanyaji wa Mapato. Mapato tunayokusanya hivi sasa yanaonekana wazi kwamba yanaweza kuisaidia Serikali, lakini ni wazi kabisa kuona kwamba jitihada hizi zinapaswa kuendelezwa na kukuzwa. Hivyo katika kuendeleza vyombo hivi sasa vilivyokuwepo vya *ZRB* na *TRA* nataka tuelewe wazi kwamba sheria zilizopo za kuanzisha vyombo hivi ndio zinazopelekea taratibu za kupata mapato yao vyombo vile vya matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya Mhe. Abdalla Maulid Diwani kuona kwamba kwa nini *TRA* na wao hawapatiwi angalau asilimia mbili au tatu ili zitoke kwenye mfuko wa Serikali katika mapato wanayoyakusanya waweze kupelekewa katika matumizi yao. Sheria ya mwaka 1996 Sheria ya Nam. 11 ya kuunda *TRA* imeweka wazi namna gani watakavyopata mapato hayo na sheria ya *ZRB* Sheria Nam. 7 ya mwaka 1996 nayo imeweka wazi namna gani ilivyoundwa Bodi ya Mapato na namna gani inaweza ikapata matumizi hayo. Kwa hivyo, si suala zito la kuonekana kwamba *TRA* wao lazima wapate mapato hayo yanayotokana na makusanyo yao kwa vile utaratibu wao unaweza ukawa unajitosheleza kupitia sheria zao za *TRA*.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa kipengele kidogo kinachoweza kuongeza mapato ya Wizara ya Fedha kupitia taasisi zake. Jana tulikuwa wengi mashuhuda tulipoisikiliza bajeti ya upande wa wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mengi tumeyaona yameelezwa yenye kufanikisha lakini nataka nieleze wazi kwamba serikali na hususan kupitia Wizara yangu ina jitihada za wazi kuhakikisha kwamba inaweza sasa hivi kuandaa chombo maalum cha kuweza kuyaratibu na kuyatangaza

yale mazuri yote yanayofanywa na serikali hii na kuweza kufikishwa kwa wananchi pale wakati yanapofanyika.

Ni wazi kwamba serikai hii inafanya mambo mengi sana mazuri lakini jitihada za kuyafikisha masuala yale kwa wananchi bado inaonekana haijapewa kipaumbele kikubwa na bado ni ndogo. Hivyo serikali tutatumia vyombo vyetu vya habari, mitandao iliyokuwepo ili kuonesha yale mambo mengi yanayofanywa katika kutekeleza ilani na kutekeleza mipango na dira ya serikali hii katika kuwaelewesha wananchi nini kinafanyika. Ni jana tu tulishuhudia kwamba kuna baadhi ya kodi zinaunganishwa na kodi nyengine. Nataka nieleze wazi kwamba serikali yetu imefanya zamani hayo na sasa hivi nikujulishwa tu wananchi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nilikuwa nataka nichangie juu ya gharama zinazopatikana na serikali. Serikali inatoa gharama nyingi kusomesha wataalam. Ni wazi kwamba wataalam wale wanapokwenda nje ya nchi au ndani ya nchi kupata elimu, ujuzi na maarifa ni mategemeo makubwa ya serikali kuja kutumika hapa ili kuiwezesha serikali nayo kuweza kupata mapato na kuendeleza jitihada zake za kuwaletea maendeleo wananchi. Ni vyema sasa serikali nayo tukaanza kujipanga na sisi tunaamini tunaweza kujipanga katika hili ili kuwatumia wataalam na hususan wazalendo ambao wamo katika taasisi zetu na wapo tayari kufanya kazi katika kuliletea taifa hili mapato mazuri kabisa na ni mapato yanayoweza yakatosheleza kama tunavyoona jitihada za upandaji wa mapato kutoka mapato ya tarakimu zile za bilioni mpaka kufikia tarakimu ambazo sasa tunakwenda nazo za trilioni.

Mhe. Naibu Spika, niwapongeze sana na nimalizie kwa kuwapongeza sana wafanyakazi wote ambao wanasimamia kukusanya mapato hususan wafanyakazi walioko katika mawizara na wafanyakazi walioko katika taasisi zinazojulikana kama ni vyombo maalum vya kukusanya kodi. Jitihada zaidi zinazofanywa

na wafanyakazi ambao wanaelimisha elimu ya kodi ni wazi nchi yetu ikielewa mfumo wa kulipa mapato na mfumo wa kulipa kodi na elimu ya kodi inapoingia katika utendaji wetu wa kazi na ukusanyaji wetu wa mapato pamoja na ufanyaji wetu wa biashara, basi ni wazi kwamba nchi hii ina uwezo wa kukusanya kodi kubwa na serikali itakuwa haimo katika mashaka ya kutegemea utegemezi zaidi wa mapato yanayotoka nje zaidi ya yale mapato tunayoyakusanya sisi wenyewe hapa.

Mhe. Naibu Spika, pongezi zangu za dhati niwapongeze wale wote wanaotoa elimu ya kodi ambao wana nia kabisa ya kuifikisha nchi hii kuweza kulipa kodi kwa hiari badala ya mivutano inayopita sasa hivi.

Mwisho kabisa nimalizie mchango wangu huu kwa kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa namna anavyosimamia sekta zote za ukusanyaji wa mapato, lakini vile vile anavyozisimamia sekta za matumizi ya mapato yanayokusanywa. Naamini wazi jitihada zake zitaipeleka hatua kubwa Serikali ya Mapinguzi ya Zanzibar katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache na kwa vile naona muda wako umeubana sana hata kama tuna mengi ya kuchangia na kueleza wananchi naomba niishie hapo. Ahsante sana naunga mkono hoja mimi na wananchi wangu walionichagua wa Jimbo la Amani pamoja na vijana wote ambao wamemchagua Dkt. Ali Mohamed Shein kwa asilimia kubwa kabisa tunaunga mkono hii hoja na tunaomba ipite kwa asilimia mia.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa nakushukuru. Mhe. Jaku Hashim Ayoub umeniomba dakika tano naomba uzitumie hizo hizo dakika tano, halafu Waziri Castico na yeye ameniomba dakika tatu na yeye nitampa. Kwa hiyo Mhe. Jaku karibu sana.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi bila ya kupoteza muda naomba nimtakie kila la kheri Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na baadhi ya watendaji wake sio wote kwa jitihada wanazozifanya katika jukumu hili.

Mhe. Naibu Spika, nitakuwa sijamfanyia haki Naibu Kamishna wa *TRA* kwa jinsi anavyofanya kazi bila ya kumbagua mtu na utendaji wake uliokuwa umetukuka. Kamishna endelea na kazi na msimamo wako bila ya kujali huyu nani, huyu nani. Kazi unayoifanya sisi tunaiona si wa juzi wala jana vyenginevyo kiti kile ungekuwa umeshaondoka zamani lakini umakini wako na utendaji wako ndio uliokufikisha hapa.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Rais vile vile kupitia kwa Waziri wa Fedha kwa msamaha alioutoa katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan kuhusu tende, unga wa ngano na sukari, tuwapongeze sana kwa hilo na hii ndio kuwafikiria wananchi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nije katika kilio cha wafanyabiashara, mzigo kutoka Zanzibar kupelekwa Tanzania Bara kwa ndugu zetu wa damu. Ninavyojua mimi Tanzania ni moja na Tanzania inaitwa kutokana na Zanzibar ndio ikaitwa Tanzania, *TRA* ni moja, *formula* ni moja, vigezo ambavyo wanavyotumia ni vimoja. Lakini kumekuwa na ubaguzi wa hali ya juu, mzigo unaotoka Msumbiji, Kenya, Zambia, Rwanda ukiingia Tanzania Bara hauna tatizo lolote. Mzigo unaotoka hapa tu karibu kutoka Zanzibar ukaupeleka pale utafikiri umepeleka kitu gani cha ajabu. Hebu tueleze hasa faida hii ya upande mmoja tu ina maana gani.

Wafanyabiashara wadogo wadogo wamekuwa wakinyanyaswa sana katika Bandari ya Dar es Salaam wakifika wananyang'anywa vitu na vinatiwa ndani. Ni aibu, tena ni aibu, *TRA* ni moja,

Tanzania ni moja, *formula* ni moja, vigezo vimoja, watu wananyanyaswa kupita kiasi. Kila siku kilio hichi kipo na kinaendelea.

Mhe. Naibu Spika, kuna kadhia ndogo tu hii ya pesa zilizopotea pale Darajani za kodi, Mhe. Haji Omar Kheri aliponijibu swali likaleta utata siku moja humu ndani akanambia milioni 66 tu zilizopotea kwa mwaka. Nikamwambia hizo pesa ni kama za ufyagizi tu kwa Manispaa maduka yaliyovunjwa Darajani serikali haijawa tayari kujengwa, zimepotea pesa chungu nzima za kodi.

Ndio ile hadithi niliyosema ya nyoka wa mdimu hukaa kwenye mdimu, ukenda kuchuma anakurukia wakati zile ndimu yeye hana kazi nazo. Leo mwaka wa pili unakwenda pale, hebu nambie tumefanya nini. Mipango haijawa tayari, ndio mipango yetu serikali siku zote, huu mwaka wa pili unakwenda zake na watatu utakwenda zake. Duka moja tu pale linaleta kontena sita kwa mwezi. Hebu nambie maduka mangapi tumeyavunja pale, pana kodi ngapi pale. Pesa tunazipoteza kiholela bila ya kuwa na mipango makini, pesa zilizopotea pale sio kidogo.

Mhe. Naibu Spika, bila ya kupoteza muda niwaombe wenzangu *ZSSF*, naomba tena *ZSSF* lile jengo waachieni jamaa wale Wakaguzi wa Majengo afisi ndogo Michenzani mpaka mtakapokuwa tayari, nyinyi nyote serikali, mnataka kuwaondosha wale jamaa hawajui waende wapi. Mmewapa sehemu chumba sijui kimoja pana afisi nne pale karibu. *ZSSF* nakuombeni sana kuomba sio kosa, kuiba ndio kosa. Waachieni jamaa wale Afisi ya Majengo kuna afisi karibu nne pale hatujaiona ramani, hatujaona chochote, watapata shida watu wale, waachieni mpaka mtakapokuwa tayari. Lakini vyenginevyo muwaondoshe pale pabaki patupu haiwezekani na wale watu wa Shirika la Umeme na wao waachieni watuuzie umeme mpaka tuone ramani zenu isijekuwa kama hadhithi ya Darajani tumevunja mipango haipo na leo huku tunaambiwa vyengine.

Mhe. Hamza Hassan Juma kazungumza skuli inayotaka kujengwa pale Rahaleo. Rahaleo pana msongamano mkubwa wa kituo cha daladala, huku tunasema nguruwe haramu, huku mchuzi wake tunaunywa, sio kitu cha maana. Msongamano uliokuwepo Darajani pale kituo cha daladala na huku twende tena kwenye kituo cha daladala na skuli zipo pale tunafanya nini, watu wanatuelewa wananchi wanatuona tunachokizungumza humu ndani.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutoka hapo nije kwenye *ZRB*. Mhe. Waziri juzi nilikuuliza swali na nikakwambia kwamba kuna ushahidi utaupata na nitauleta Mungu akitujaalia kama yeye mwenyewe yupo. *ZRB* kazi mnayoifanya sio mbaya lakini sasa kumekuwa kuna mateso, mzigo unapita bandarini Zanzibar kwenye jahazi. Juzi imetokea kadhia ya mafuta yamepakiwa kufika kule mbele KMKM wakaikamata boti wakairudisha na mtu ana *transfer* yake na vibali vyote akatoleshwa milioni 10. Hii dhambi na uonevu, hatuwezi kwenda mbele kwa mambo kama haya. Tunapanga mipango hatuko tayari.

Mhe. Mwenyekiti, *ZRB* walikuwa wakikamata watu nje kwa mafuta wakati sheria hawana. Baada ya kuleta sheria hapa, kuna Kamishna jamaa mmoja wa kihindi Mohammed Hashim nikamwambia utapata shida tafuta njia kwanza (*formula*), akaleta *formula* akatafuta kwenye vyombo, alikuwa akirukia tu. Ndio nikasema hii nchi ina taratibu na sheria zake.

Mhe. Naibu Spika, baada hapo mimi nafikiri mchango wangu nitamalizia hapa na kidogo nimalizie kuhusu *ZRB* tena. Chumba kimoja sasa hivi wafanyakazi zile hoteli zinazokwenda haziendi, mishahara ya wafanyakazi haitoki, wanapiga kelele wenye hoteli, kichwa kimoja kuchukua dola tisa mtu anakodisha shilingi elfu 20 angalau apate mshahara wake, hichi kitu mkakiangalie. Ikiwa Hayatt Hotel dola tisa mfano wake na huyu mlala hoi mwenye

hoteli yake dola tisa hapana. Mtoto hazaliwi akenda mbio siku hiyo hiyo kwanza hutambaa, akakamata kiambaza akaanguka.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Jaku Hashim Ayoub malizia.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa muda ulionipa, lakini hii dola tisa Mhe. Waziri liangalie haiwezekani hoteli ya juu ikawa milioni tisa na hoteli ya chini ikawa dola tisa kwa kichwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:** Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa na mimi nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii nyeti katika Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kwa kumpongeza Mhe. Rais wetu Ali Mohamed Shein kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu katika mazingira mazuri ya amani, utulivu, hata tunapokuwa tunapata maendeleo yote tunayapata ni kwa sababu ya amani hiyo. Naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuendelea kusimamia vizuri shughuli zote za serikali na utendaji wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mawaziri wote.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia baada ya Waheshimiwa Wajumbe kwa busara zao za ushauri katika maeneo ambayo walihisi yanahitaji kutiliwa mkazo ili mapato yawe mengi. Aidha, niungane na wale wote waliompongeza Mhe. Mwakilishi wa Donge Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed kwa kazi zake nzuri kwa kujitolea kuwahudumia watu wake licha ya kuwa na kazi nyingi sana za wizara ambazo wizara yake imebeba kama idara kumi na kati ya hizo kuna taasisi nyengine zinazojitegemea zile za Muungano zinazofanya kazi

Zanzibar. Kitu ambacho sio cha kawaida kama mtu asipofanya kazi kwa bidii hawezi kukidhi mahitaji.

Mhe. Naibu Spika, kama unavyojua kuwa ukitaja Wizara ya Fedha unataja uti wa mgongo wa utekelezaji wote wa nchi. Inaonesha wazi kuwa kumbe nchi ikisimamia ukusanyaji mzuri wa mapato hatuwezi kuwa wanyonge kwa kuwa unyonge hujitokeza pale ambapo una mipango mikubwa lakini fedha huna, basi huishia kuomba.

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda kuendelea kuwatia moyo watendaji wote wanaofanya kazi katika wizara hii kwa kazi zao nzuri wanazozifanya ambazo kwa hilo ndio maana tunaweza kuendelea kupata mapato mengi ya kutosha. Ndio maana inaendelea kumpa moyo Mhe. Rais wetu kuendelea kuwa na moyo wa kuchangia na moyo wa kuwafikiria wananchi wake hasa wazee ambao wanapata pencheni, ukiangalia mpaka sasa hivi tuko kwenye rekodi ya kimataifa ya kuona kwamba pencheni inayotolewa kwa Zanzibar inakuwa ni ya kihistoria. Kwa sababu kwa mapato tunayochangia ni mengi kiasi tunachopata na pesa zinazotolewa ni nyingi. Laiti tusingeweza kuchangia tusingethubutu hata siku moja kutoa huduma hiyo kwa wazee na sio ya wazee peke yao pia tunapata faraja kubwa katika suala la afya.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi afya nikizungumzia suala la wanawake na watoto wanapata faraja kubwa. Eneo walilojengewa la hospitali na mahali wanapotibiwa, wazazi wanapokwenda kuzalia ni sehemu ambayo inatia heshima. Tunaamini kabisa watoto wakizaliwa katika mazingira yale tunawapa maisha mazuri.

Pia tukija kwenye suala la elimu bure, elimu ni msingi wa maisha, anasema mshike sana elimu kwa maana ni sehemu ya maisha yako. Kila mtoto anaambiwa mng'ang'anie sana elimu. Elimu

imeanza kuonekana kabisa na jinsi ambavyo watoto wengi walikuwa hawawezi kwenda shule sasa hivi kila mtoto anakwenda shule ni kitu ambacho tunaendelea kumpongeza Mhe. Rais na kumuombea maisha marefu.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la maji kulikuwa kuna kipindi ambacho maji yanasumbua sana. Maji yanapatikana kama tu mapato yataweza kuwa mazuri. Kuna suala la umeme, kuna huduma za kilimo ambazo sasa hivi kutokana na hali halisi kuna watu wengi katika suala la sekta ya ujasiriamali wanajitegemea katika kutumia masuala ya elimu na kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kuna chombo cha habari ambacho kinatoa taarifa zinazohusiana na wizara mbali mbali hasa pia kwenye Wizara yangu ambayo inasaidia sana katika kuelimisha watu kuhusiana na masuala ya udhalilishaji wa kijinsia. Pia masuala mengine yanayohusiana na masuala ya malezi mazuri kwa watoto na jinsi gani yanaweza kuwashawishi watu, yote haya hayawezi kufanyika kama hakuna pesa za kutosha.

Lakini pia kuna suala zima la ulinzi tunashukuru sana na kuipongeza serikali yetu kwamba ulinzi unaendelea kuwa mzuri na tuendelee kuwatia moyo hao ambao wanafanya kwa sababu makusanyo ni mazuri. Kwa namna hiyo tuunge mkono hotuba hii ya Wizara ya Fedha ipate kuendelea kujenga nchi katika amani na utulivu na uwezeshaji wa wanawake na vijana utekelezaji ukiwa tu pato litakuwa ni zuri mpango huu mzuri utasaidia sana katika suala zima la kupiga vita suala la udhalilishaji kwa watoto na akina mama na hata vijana katika mazingira mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, napenda niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa ajili ya wizara hii.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante sana Mheshimiwa sasa nimpishe Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya kuja kujibu hoja za Waheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, afya na uzima na kutuwezesha kuendelea na majukumu yetu katika Baraza la Wawakilishi kwa mafanikio makubwa.

Namshukuru sana Mhe. Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutuongoza vyema katika nchi yetu na kwa miongozo anayotupatia katika wizara jambo ambalo limeweza kutusaidia katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku. Vile vile naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi ambaye ndio Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali hapa Barazani kwa miongozo na maelekezo yake mazuri ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa sana mafanikio ya Wizara yetu.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru wewe pia na namshukuru Mhe. Spika na Wenyeviti wote kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika kuliongoza Baraza letu hili lakini hasa katika kuongoza Baraza katika mijadala yote ya bajeti za Mawizara mbali mbali na Wizara yetu ya Fedha na Mipango miongozo ambayo ilitolewa kwa umakini na ufanisi mkubwa. Nawapongeza na kuwashukuru sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa aina ya pekee naomba uniruhusu nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni pamoja na Wajumbe wake wote kwa maoni yao ya upeo ya Kamati yaliyosomwa kwa niaba yake na Mhe. Ussi Yahya Haji, Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni.

Aidha, nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza kwa mashirikiano mazuri na Wizara yangu na wale waliopata fursa ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara yangu waliopata kusema moja kwa moja na wale waliochangia kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, wajumbe waliochangia hotuba ya Wizara yangu ni 35 kwa ujumla wake, 25 walichangia kwa kusema moja kwa moja na waheshimiwa 10 walichangia kwa maandishi. Kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, naomba kuwataja waliochangia kama ifuatavyo:-

Waliochangia kwa kusema moja kwa moja ni:

1. Mhe. Ussi Yahya Haji Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni
2. Mhe. Ali Salum Haji Mnadhimu wetu wa Chama cha Mapinduzi na Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani
3. Mhe. Ali Suleiman Ali Mwakilishi wa Jimbo la Kijitoupele
4. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil Uteuzi wa Mhe. Rais
5. Mhe. Simai Mohammed Said Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu
6. Mhe. Hidaya Ali Makame Viti Maalum Vijana wa Mkoa wa Kaskazini Unguja
7. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Mwakilishi wa Jimbo la Mtopepo
8. Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Jimbo la Shaurimoyo
9. Mhe. Ali Hassan Bakari Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe
10. Mhe. Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa Jimbo la Welezo
11. Mhe. Omar Seif Abeid Mwakilishi wa Jimbo la Konde

12. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu Mwakilishi wa Jimbo la Mtoni
13. Mhe. Mohamed Said Mohamed Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae
14. Mhe. Panya Ali Abdalla Viti Maalum Wanawake Mkoa wa Kaskazini Unguja
15. Mhe. Suleiman Sarahan Said Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake
16. Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe
17. Mhe. Miraji Khamis Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni
18. Mhe. Maryam Thani Juma Mwakilishi wa Jimbo la Gando
19. Mhe. Suleiman Makame Ali Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani
20. Mhe. Said Soud Said Waziri Asiye na Wizara Maalum (Uteuzi wa Mhe. Rais)
21. Mhe. Juma Ali Khatib Waziri Asiye na Wizara Maalum (Uteuzi wa Mhe. Rais)
22. Mhe. Salama Aboud Talib Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji, Nishati na Mazingira
23. Mhe. Rashid Ali Juma Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo
24. Mhe. Maudline Cyrus Castico Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
25. Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Paje

Waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Abdalla Ali Kombo Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe
2. Mhe. Rashid Makame Shamsi Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni

3. Mhe. Mussa Ali Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Ole
4. Mhe. Shaib Said Ali Mwakilishi wa Jimbo la Chonga
5. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwakilishi wa Jimbo la Dimani
6. Mhe. Tatu Mohamed Ussi Viti Maalum
7. Mhe. Shamata Shaame Khamis Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni na Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
8. Mhe. Mauldile Cyrus Castico Alichangia kwa maandishi
9. Mhe. Shehe Hamad Mattar Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni
10. Mhe. Mgeni Hassan Juma Naibu Spika

Moja ilikuja haina jina lakini naomba kumtambua alitoa mchango kwa maandishi.

Naomba kusahihisha Mhe. Naibu Spika, jina la Mhe. Simai Mohammed Said nililitaja kwa makosa, sasa ifahamike kwamba ni Simai Mohammed Said.

Mhe. Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata nafasi ya kuchangia kwa michango yao mizuri na niseme michango yote, maoni yote tumeyapokea kwa moyo mkunjufu kabisa, yale yanayohitaji kufuatiliwa tutayafuatilia kwa umakini na yale yanayohitaji kuzingatiwa tutayazingatia. Lakini yapo mambo ambayo yatahitaji ufafanuzi kidogo na kwa ruhusa yako Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa ufafanuzi huo kama ifuatavyo.

Michango iliyotolewa na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Mhe. Naibu Spika, kamati imeitaka Wizara ya Fedha na Mipango iharakishe mchakato wa ununuzi wa mashine za *EFD* suala hili

pia lilizungumziwa na Mhe. Omar Seif Abeid. Naomba kuwajulisha Waheshimiwa Wajumbe wote kuwa tupo katika utaratibu wa ununuzi wa mashine hizo tunashirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika ununuzi wa vifaa hivyo vya *EFD* na tunatarajia kwamba mashine hizo zitakuwa tayari ndani ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Kamati pia ilitaka Wizara isikate tamaa kuhusiana au kuhamasisha washirika wa maendeleo na iongeze kasi ya ufatiliaji wa pesa kwa miradi wa ujenzi wa *terminal II* katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

Waheshimiwa Wajumbe nataka nikuhakikishieni kwamba Serikali yetu ina mahusiano mazuri na washirika wa maendeleo na tunazidi kuwasiliana nao ili wazidi kuchangia katika harakati za maendeleo katika nchi yetu. Serikali inatoa kipaumbele katika kulimaliza jengo la *terminal II* na tupo katika hatua ya kufanikiwa kuukwamua ujenzi huo ambao tunatarajiwa utaanza tena mapema katika robo ya kwanza ya mwaka wa 2017/2018. Aidha, Kamati imeitaka Wizara ikamilishe taratibu zilizobaki kwa mwekezaji wa Hoteli ya Bwawani ili kukamilisha ujenzi huo na Serikali iweze kupata mapato yake na kupatikana kwa ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, Wizara imepokea ushauri huo na jitihada zaidi zinachukuliwa, niwajulishe tu Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba vikao mbali mbali na mwekezaji huyu tayari vimefanyika kuzungumzia changamoto za mradi na makubaliano yameshafikiwa. Ni matumaini yetu kwamba mwekezaji huyu si muda mrefu kutoka sasa ataanza kuchukua hatua kwa yale yote tuliyokubaliana na kuendeleza mradi huo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Fedha na Mipango pia ilitakiwa iwafikirie kuwapatia posho la mazingira magumu Wasaidizi

Wahasibu Wakuu wa *Vote*, Wakaguzi wa Ndani wa *Vote* na Washika Fedha wa *Vote*.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwamba wafanyakazi hawa wanafanya kazi muhimu sana na katika mazingira yenye vishawishi vikubwa. Hata hivyo, nieleze kwamba kwa kiasi kikubwa Serikali imeamua kudhibiti matumizi ya maposho mbali mbali kwa wafanyakazi wa Serikali. Tunachukua ushauri wa kamati na tutazungumza na Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora juu ya ushauri huu ili kuangalia uwezekano huo.

Kamati pia ilishauri Wizara kuweka utaratibu maalum wa kupandisha madaraja Wahasibu, Washika Fedha na Wakaguzi wa Ndani. Naomba nikueleze kwamba ni hivi karibuni tu wafanyakazi wote wa Wizara na Idara za Serikali wamewekwa katika madaraja yao kulingana na sifa zao na Muundo wa Utumishi *(Scheme of Service).* Upandishaji vyeo kwa wafanyakazi utafanyika kwa kuzingatia *Scheme of Service* lakini pia vile vile nafasi zitakazojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, Kamati pia ilishauri Wizara ya Fedha na Mipango iongeze pencheni kwa wastaafu, swali hili pia liliulizwa na Mhe. Mohamed Said Mohamed na Mhe. Suleiman Sarahan Said. Waheshimiwa Wajumbe naomba nieleze kwamba suala hili limefanyiwa kazi sambamba na mapitio ya mishahara mipya, Serikali itatoa kauli juu ya jambo hili katika hotuba ya Serikali inatakayosomwa tarehe 12 Juni, 2017. Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wenzangu nawaomba sote tusubiri siku hiyo na kauli ya Serikali itatolewa juu ya jambo hilo.

Mhe. Ali Khamis Bakar nae alizungumzia suala la kucheleweshe kulipwa kwa mafao ya wastaafu. Naomba kumjulisha kwamba pencheni za wastaafu zinalipwa kila mwezi na hazicheleweshwi. Kwa kawaida inalipwa kati ya tarehe 24 hadi tarehe 1 ya kila

mwezi. Kuhusu kiinua mgongo Serikali hadi sasa imeshalipa viinua mgongo kwa wale wote ambao fomu zao zimekamilisha mchakato wa malipo hadi kufikia mwezi wa Disemba, 2016. Hivi sasa zipo fomu zenye jumla ya shilingi bilioni 2.708 ambazo zinatarajiwa kulipwa ndani ya mwezi huu ambazo zitakuwa ni fomu zilizowasilishwa na kukamilisha mchakato wa malipo hadi mwezi Februari, 2017. Serikali itaendelea kulipa viinua mgongo pale tu fomu za wahusika zitakapokamilisha taratibu zote husika za malipo. Serikali inawajali sana wastaafu na itaendelea kulipa mafao yao kwani wao ni sehemu muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Wizara pia imetakiwa na Kamati kuongeza ada ya Mfuko wa Barabara *(Road Fund)* kutoka shilingi 100 hadi shilingi 150 kwa mita kwa mwaka 2018/2019. Suala hili pia lilizungumziwa kwa hisia na Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Mohamed Said Mohamed. Niseme tunaupokea ushauri wao na tutaangalia uwezekano huo katika bajeti kwa mwaka 2018/2019. Hata hivyo, kwa sasa mkazo wa Serikali si kuongeza viwango vya kodi bali ni kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi kutokana na vyanzo ambavyo tunavyo hivi sasa na hilo tunalifanya makusudi ili kuwaondoshea mzigo mkubwa walipa kodi, lakini vile vile kuwaondoshea mzigo na makali wananchi wetu, lakini pia katika kuchochea ukuaji wa uchumi katika nchi yetu.

Kamati imeitaka Wizara kusimamia kwa karibu ujenzi wa ukuta pale Forodhani na mradi huu nieleze tu upo katika hatua za mwisho kukamilika na matarajio yetu kwamba utakamilika ndani ya robo ya kwanza ya mwaka 2017/2018. Mheshimiwa Kamati pia ilitaka Wizara itumie Mradi wa *ZUSP* kuondoa maji ya mvua katika eneo la Mwanakwereke, Kibondemzungu na Kiembesamaki katika barabara ya kwenda Uwanja wa Ndege.

Mhe. Naibu Spika, Mradi wa Huduma za Mji *(ZUSP)* unafadhiliwa kwa mkopo nafuu wa Benki ya Dunia maeneo haya

matatu ambayo yametajwa na kamati hayakuwemo katika maeneo yaliyokubaliwa kuingizwa katika mradi huu hapo awali. Lakini kwa mazingira maalum na kwa maombi maalum eneo la Mwanakwerekwe limeingizwa katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi huo ambao utatekelezwa sambamba na ujenzi wa jaa jipya na la kisasa huko Kibele na kwa hivyo eneo la Mwanakwerekwe linakuwemo katika awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa *ZUSP*.

Ushauri kwa Wizara kushughulikia Shirika la *ZAFICO* na kukamilisha nyumba za makaazi Mbweni, Jumba la Treni na *Shopping Mall* Michezani, makontena kupitia *ZSSF*, ushauri huu tunaupokea na haya yote yaliyozungumzwa tutayazingatia.

Mhe. Naibu Spika, kamati na wajumbe wengi waliochangia walizungumzia suala la msongamano mkubwa katika Benki ya Watu wa Zanzibar hasa katika siku za mwisho wa mwezi na wakati wa malipo ya pencheni na mwisho wa mwaka wakati wananchi wanapasisha vyombo vyao vya usafiri. Miongoni mwa waliochangia suala hili ni:

1. Mhe. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Hidaya Ali Makame
3. Mhe. Omar Seif Abeid
4. Mhe. Ali Khamis Bakar
5. Mhe. Shamata Shaame Khamis
6. Mhe. Suleiman Makame Ali

Naomba niwajulishe Waheshimiwa Wajumbe kwamba ni kweli Benki ya Watu wa Zanzibar hujaa katika siku za mwisho wa mwezi ambapo wateja wengi wamekuwa wakitumia huduma za benki kupitia kidirishani. Aidha, kumekuwa na foleni kubwa katika mashine za *ATM* zilizopo katika maeneo mbali mbali katika Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Kwa kuzingatia hilo

Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Watu wa Zanzibar inachukua hatua zifuatazo:

1. Moja kuongeza idadi ya *ATM* Unguja na Pemba ambapo maeneo kama Micheweni, Mahonda, Nungwi yanafikiriwa kuwekewa huduma hiyo ya *ATM*.

2. Lakini pili kuunganisha mfumo wa Benki na Taasisi mbali mbali za Serikali ikiwemo *ZRB, ZAWA, ZECO,* Bandari, Mahkama na Hospitali ili walipa kodi waweze kufanya malipo na kutumia *ATM* na simu bila ya kwenda benki. Kwa hivyo huduma hiyo inazingatiwa. *(Makofi)*

3. Lakini pia benki inadhamiria kuanzisha *Agency Banking* kwa maana Benki ya Uwakala ambapo wakala mbali mbali walioko mitaani wataweza kupokea amana za wateja na kufanya malipo kwa wateja. Utaratibu huu utapunguza gharama katika kuendesha matawi ya benki na kupunguza foleni za wateja katika matawi yaliopo. Haya yote yataenda pamoja na mabadiliko ya *Core Banking System* ambayo nilikwisha kuyaelezea hapa Mhe. Naibu Spika, ambayo yataweza kuhimili ongezeko kubwa la wateja wa benki yetu hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kiwango cha riba Serikali kupitia Benki ya Watu wa Zanzibar imepunguza kiwango cha riba kwa mikopo binafsi kwa maana *Personal Loans* kuanzia tarehe 1 Mei, 2016. Aidha, kiwango cha riba kwa mikopo ya nyumba kwa wananchi imepungua hadi asilimia 14.5 hii imetokana na kupungua kwa gharama za fedha katika masoko ya fedha nchini.

Mhe. Ali Salum Haji ametupongeza na tunapokea pongezi zake, tunauchukua ushauri wa kuhimiza na kufuatilia wafanyabiashara kutoa risiti wakati wa kuuza na wateja nao kudai risiti wakati wanaponunua. Hili pia lilizungumwa na Mhe. Omar Seif Abeid na

Mhe. Shamata Shaame Khamis na wao pia walihimiza kuhusu suala hili la kutoa risiti na kupokea au kudai risiti. Hii itaendelea kufanyika kwa kuzidi kutoa taaluma juu ya umuhimu wa kodi wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu.

Aidha, watendaji wa *TRA* na *ZRB* wasiofuata maadili ya utendaji na wanaojihusisha na upotevu wa mapato ya Serikali watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo. Vile vile kwa sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma imeshapitishwa na kuanza kutumika, tumeipitisha katika Baraza hili ni sheria ya mwaka 2016 taaluma itatolewa kwa watendaji wa vitengo vya ununuzi ili kudhibiti upotevu wa fedha za umma na kupata thamani ya fedha kwa bidhaa na huduma zinazonunuliwa na Serikali.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil nae alitupongeza tunapokea pongezi hizo na pia alipongeza Mpango wa Serikali wa kujenga majengo ya Ofisi ya Serikali na ushauri wake tumeupokea na tunauzingatia. Ushauri kama huo pia ulitolewa na Mhe. Hidaya Ali Makame, Mhe. Suleiman Sarahan Said na Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Simai Mohammed Said Mwakilishi wa Jimbo la Tunguu ametoa pongezi kwa Wizara tunazipokea na ushauri wake tunauchukua ikiwemo *ZRB* kusaidia kutangaza utalii wa Zanzibar. Lakini pia alishauri kuhusiana na mavazi rasmi kwa watendaji wa *PBZ* na *ZIPA* nao pamoja na wizara kuwa karibu na wawekezaji na haya tunayachukua. Hata hivyo, naomba kueleza kwamba *target* za *ZRB* na *rate* za hoteli zinazingatia msimu *seasonality*, nyingi ya kodi zinatozwa kwa asilimia ya bei kwa maana ya *rate* wanayotoza wenye mahoteli hivyo tayari inazingatia msimu kwa maana *seasonality* ile. Tunakubali kwamba wapo wawekezaji ambao si waaminifu na kudanganya bei wanazotoza na hivyo kuathiri mapato ya Serikali, tunaahidi kufuatilia wawekezaji hao

na wale watakaokutwa na udanganyifu hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Mhe. Hidaya Ali Makame alizungumzia suala la migogoro ya ardhi, ni kweli yapo matatizo ya ardhi katika baadhi ya maeneo na katika baadhi ya miradi Serikali imeweka utaratibu wa kufutwa na wawekezaji katika kupata ardhi. Kabla ya mwekezaji kupatiwa kibali au mkataba wa ukodishwaji ni lazima afuate utaratibu huo, na utaratibu huo Mhe. Naibu Spika, ni kwanza apeleke ombi la mradi kwa maana *letter of intention* kwa *ZIPA* na kujaza fomu maalum ambayo inapatikana katika *website* ya *ZIPA.* Lakini baada ya kupatikana *ZIPA* kwa kushikiana na taasisi zote husika huwa zinafanya mikutano kujadili mradi huo zinatembelea *site* kwa pamoja lakini pia zinawashirikisha wananchi na eneo hilo na viongozi wa eneo hilo akiwemo Sheha kwa ajili ya kuondoa migongano katika matumizi ya eneo hilo. Lakini vile vile hati au cheti cha uwekezaji kinatolewa pale tu baada ya kuhakikisha kwamba fidia inayostahiki kulipwa kwa wananchi imelipwa kwa ukamilifu wake.

Mhe. Naibu Spika, waheshimiwa wametaka kuchukuliwa hatua kwa wawekezaji waliopewa *lease* ya ardhi kwa muda mrefu na kutoyaendeleza maeneo waliyopewa. Mhe. Hamza Hassan Juma, Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mhe. Hidaya Ali Makame, Mhe. Omar Seif Abeid na Mhe. Suleiman Makame Ali walilizungumzia suala hili. Naomba niwajulishe kwamba Kamisheni ya Ardhi kwa kushirikiana na *ZRB* wameyatembelea maeneo takriban yote ya wawekezaji na kungalia hata wale ambao hawalipi kodi za ardhi. Ripoti ya tathmini hiyo imekamilika na tayari ipo Serikalini kwa ajili ya kuzingatiwa. Lakini pia nieleze kwamba Sheria ya Uwekezaji ya *ZIPA* ya mwaka 2004 ndio sheria inayosimamia taratibu za upatikanaji na ufutwaji wa miradi ya uwekezaji kifungu cha 14 kifungu kidogo cha 2(b) kinatoa mamlaka ya kupata mradi wa uwekezaji ambao umeshindwa kutimiza wajibu wa kuendeleza mradi husika ambao hauna sababu ya kuridhisha

na hauna sababu za msingi. Utaratibu huo unafanywa na iko miradi ambayo tayari imefutwa kwa mnasaba huo.

Serikali kupitia *ZIPA* itafanya mapitio ya miradi hiyo na ile ambayo haina mwelekeo wa kuendelezwa Serikali haitosita kufuata sheria au kuchukua sheria ya kufuta miradi hiyo, hii itasaidia Serikali kutumia maeneo hayo kwa kuwapa wawekezaji wengine ambao hatimaye wataweza kulipa kodi ya rasilimali hiyo na kuendeleza miradi yao kwa faida ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, katika ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua naomba nitoe jawabu hili kwa Mhe. Hidaya Ali Makame lakini pia namuunganisha Mhe. Mohamed Said Mohamed, Mhe. Hamza Hassan Juma na Mhe. Miraji Khamis Mussa na kwamba maeneo yanayohusika ni kama ifuatavyo:

Tuna karibu maeneo sita ambayo yalianzwa kuendelezwa katika awamu ya mwanzo *ZUSP* na yataendelezwa mengine katika awamu ya pili ya *ZUSP* ambayo yale yaliyokuwa hayakukamilika katika awamu ya kwanza na yamegawika katika mifumo sita. Vile vile ambayo wanaita *System C* au mfumo C unajumuisha maeneo ya Jang'ombe, Magomeni, Mpendae kwa Binti Hamrani ambalo hili alilizungumza sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, Meya, Migombani na Kilimani na *System I* ni maeneo ya Darajabovu, Kwamtipura, Shaurimoyo, Chumbuni na Mwembemakumbi. *System G* ni Mtopepo na Karakana ambayo kazi hii *almost* imeshakamilika. Lakini *System B* ni Kijangwani, viwanja vya Kibandamaiti, *System F* ni viwanja vya Mnazi Mmoja ambayo kazi *almost* nayo imeshakamilika na *System C* ni Magogoni, Nyerere, Sebleni, Amani, Mikunguni, Saateni hadi Kinazini.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu maji ya bwawa la Mwanakwerekwe kama nilivyosema eneo hili tayari limeingizwa katika Mradi wa *ZUSP* awamu ya pili na tayari wizara imemtaka Mshauri Elekezi kuangalia namna gani maji yaliyopo eneo hilo yanaweza

kupelekwa bwawa la Sebleni na kuunganishwa na mtaro mkubwa utakaopeleka maji Kinazini hadi baharini kupitia Mikunguni, Kwa Juma Pweza na Saateni kwa Abass Hussein.

Mhe. Rashid Makame Shamsi na yeye alizungumzia kuhusiana na suala la mtaro wa maji ya mvua katika Jimbo la Magomeni. Nimjuilishe mheshimiwa kwamba tayari umekamilika msingi huo katika maeneo ya Magomeni, kilichobaki sasa hivi ni kuunganisha lile eneo na utaunganishwa na mitaro mingine ambayo itatoa maji lakini kinachosubiriwa sasa ni ulipaji wa fidia kwa wananchi wa eneo hilo. Nimjulishe mheshimiwa kwamba tayari fedha za kulipa fidia kwa waathirika wote wa mradi zimeshapatikana ziko tayari na wananchi walioathirika na mtaro wa Jang'ombe wameanza kuitwa kwa ajili ya kulipwa. Inatarajiwa kuwa ujenzi utakamilika ndani ya miezi sita baada ya waathirika kulipwa fidia na mkandarasi kukabidhiwa *site* husika.

Mhe. Naibu Spika, mikataba mikubwa na wakandarasi itazamwe kwa makini. Tumelipokea wazo hili pamoja na maoni ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh tutashirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuona namna ya kuimarisha zaidi usimamizi wa mikataba yetu.

Mhe. Mussa Ali Mussa wa Jimbo la Ole yeye alizungumzia suala la fidia katika barabara ya Ole/Kengeja. Nimjulishe tu kwamba fidia imelipwa kwa mujibu wa matokeo ya uhakiki. Lakini tunaelewa pia kwamba kuna malalamiko ya wananchi na serikali kupitia wizara inayohusika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji inalifanyia kazi suala hili. Tunakuomba Mhe. Mwakilishi pamoja na wananchi wa Ole wavute subra na kwa wale wananchi wachache ambao bado wana malalamiko basi malalamiko yao yatazingatiwa na kufuatiliwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma alitaka kujua hatma ya wafanyakazi wa Wizara ya Fedha na Mipango waliosimamishwa kazi kwa tuhuma za ubadhirifu wa fedha za umma. Suala hili pia liliulizwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Niseme kwamba suala hili nimeshalitolea ufafanuzi mara nyingi, lakini nitaendelea kutoa ufafanuzi huo kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Bodi ya Uchunguzi iliundwa kwa mujibu wa sheria ya fedha za umma ya mwaka 2005, na bodi hiyo iliwasilisha ripoti yake wizarani baada ya kukamilisha kazi hiyo. Suala hili nimelitolea ufafanuzi kama nilivyosema mara nyingi lakini hata hivyo hatua mbali mbali zimeshaanza kuchukuliwa ikiwemo kuwapa fursa wahusika wote kujieleza. Takriban wahusika wote wametoa maelezo yao na wote waliojieleza wamekanusha kuhusika na ubadhirifu huo.

Baada ya Bodi ya Uchunguzi kumaliza kazi yake imegundulika kwamba wafanyakazi waliohusika sasa na kadhia hii ni 22, pale awali walikuwa ni 11 ambao hao ndio waliosimamishwa kazi, lakini sasa baada ya uchunguzi imeonekana na wengine waunganishwe kwenye kadhia ile na jumla yao sasa wako 22. Lakini fedha zilizopotea kama nilivyowahi kutoa taarifa ni zaidi ya bilioni 1 lakini katika wote hao yuko mfanyakazi mmoja ambaye bodi haikuweza kumuhusisha moja kwa moja na kadhia hii. Kwa hivyo, kwa mfanyakazi huyu ambaye hakuweza kuhusishwa moja kwa moja, wizara tayari imeshachukua hatua ya kumrejesha kazini. Kwa hivyo, wale waliobaki ambao wamekanusha uchunguzi unaendelea na vyombo vinavyohusika vimekabidhiwa suala hili. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe tuvute subra bado wakati suala hili linashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kupatikana kwa *payee* kwa wafanyakazi wa SMT wanaofanyia kazi hapa Zanzibar. Nieleze tu

kwamba malipo ya *payee* yanapatikana kwa ukamilifu na tayari fedha hizi zimelipwa hadi mwezi wa April, 2017 na malipo ya Mei yanatarajiwa kulipwa hivi karibuni.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu *x- ray machine* kwa Uwanja wa Ndege na Bandari nieleze kwamba mradi wa *CCTV* unanunua *x-ray machine* kubwa nne kwa ajili ya bandari ya Malindi na Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma pia alitaka kujua kwa nini fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo zimepatikana chache. Niseme ni kweli *observation* yake lakini sababu hii ya kuchelewa inatokana na sababu ya kuchelewa kwa taratibu za kuendeleza na kuanza utekelezaji wa miradi mikubwa ikiwemo ujenzi wa jengo la *Terminal II* katika Uwanja wa Ndege na utekelezaji wa Mradi wa *E-Government* na Mradi wa Bandari ya Makontena pale Mpigaduri.

Mhe. Naibu Spika, suala la Mradi wa Kiwanda cha Nondo ambalo pia lilizungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, tukiri kupokea ombi la mradi la wawekezaji kutoka Canada na Tanzania. Mradi huu ni wa viwanda vikubwa kwa maana ya *heavy industry* na eneo alilotaka mwekezaji kuekeza mradi huu ni katika maeneo huru ya Fumba ambapo ardhi yake kwa mujibu wa *master plan* haijawekwa kutumika kwa viwanda vikubwa vya nje.

Mhe. Naibu Spika, mpango huu umetengewa eneo la hekta 102 kwa mujibu wa *Fumba Master Plan*, na ni kwa ajili ya mtaa wa viwanda vidogo vidogo *light industry* vitakavyohusisha viwanda vya usindikaji mazao ya kilimo, mazao ya baharini na mifugo, viwanda vya kufunganisha kwa maana ya *assembling factories*, viwanda vya kutengeneza *package* kwa maana *packaging material* na *ICT* ndio eneo hili, lakini ni kiwanda muhimu. Tunachoshauri ni kwamba wizara inayohusika na maendeleo ya

viwanda italiangalia suala hili na kuona ni eneo gani muafaka wa kuwa na kiwanda cha aina hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Omar Seif Abeid alitaka kujua ni kiasi gani cha mapato kinakusanywa kutokana na kodi ya mafuta. Nimjulishe Mhe. Omar Seif Abeid kwamba uingizaji wa mafuta hadi mwezi wa Mei, 2017 ni lita milioni 134.9. Kwa Unguja ilikuwa ni lita milioni 120.1 na Pemba lita milioni 14.8, na jumla ya shilingi bilioni 52.9 zilikusanywa na *ZRB* ikiwemo tozo ya miundombinu, tozo ya biashara, tozo ya *petroleum* na *road license*. *TRA* kwa upande wake ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 6.5, hivyo mapato yote yanayotokana na mapato ya mafuta ni shilingi bilioni 59.4.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la usajili wa walipa kodi, suala hili nimeshalitolea maelezo ndani ya Baraza hili. Lakini niseme tu jitihada zaidi zitachukuliwa ili kuona wote wanaostahiki kusajiliwa kama walipa kodi wanasajiliwa kwa ukamilifu wake. Aidha, *ZSSF* itaendelea kufuatilia waajiri wote na kuona kwamba wanajisajili wao wenyewe kama waajiri lakini wanawasajili waajiriwa wao katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na wanatekeleza wajibu wao wa kutoa michango kama ilivyoelezwa na sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) yeye alizungumzia suala la gawio la *BoT*, suala hili pia liliulizwa na Mhe. Miraji Khamis Mussa. Ni kweli mwaka 2016/2017 tulipanga kupata shilingi bilioni 4 na hadi mwezi wa Machi, 2017 fedha hizo zilikuwa hazijapatikana. Lakini kwa furaha kubwa naomba kumjuilisha Mhe. Dimwa kwamba gawio la *BoT* limepatikana katika robo ya nne ya mwaka huu wa fedha unaomalizika 2016/2017 na fedha zilizopatikana ni bilioni 14 sisi tulitarajia bilioni 4 lakini tumeenda kupata bilioni 14 ni zaidi na zaidi ya tulichokitarajia.

Mhe. Naibu Spika, Mswada wa Sheria ya Ushuru wa *Stamp* ambayo inatarajiwa kusomwa kwa hati ya dharura katika kikao hiki inapendekeza kuwa na utaratibu mzuri wa kisheria wa kulipa kodi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. Aidha, mfumo mzima wa kodi utafanyiwa mapitio katika mwaka wa fedha 2017/2018 ili kuweka mfumo bora wa kulipa kodi kwa hiari kwa walipa kodi wote nchini.
Pia Mhe. Mohammed Said Mohammed alizungumzia kuhusiana na *figure* zilizokuwepo katika jadweli Nam. 3 katika ukurasa wa 50 kwenye kitabu. Naomba kueleza tu kwamba zile *figure* zina makosa tuombe radhi kwa hilo na *figure* sahihi tutazitoa baadae na tutampatia Mhe. Dimwa ili aweze kujua ni marekebisho gani yamefanyika.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kifungu cha SF010104 kinachohusika na usimamizi wa hesabu za ndani katika *budget estimate*. Fedha zilizowekwa kwa mwaka 2017/2018 ni shilingi bilioni tatu na milioni thalathini na tatu, wakati kwa mwaka 2016/2017 fedha zilizotengwa zilikuwa ni shilingi milioni mia saba na ishirini laki nane na thamanini na moja elfu. Ni kweli *figure* hizo na hii niseme inatokana na sababu kwamba hivi sasa tumeamua kuunda idara mpya ya ukaguzi wa ndani, pale mwanzo Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ilikuwa shughuli hizi za Idara ya Ukaguzi wa Ndani zimeunganishwa pamoja, sasa tume-*separate* na kuwa na idara mbili. Kwa hiyo, tumeunda idara moja mpya ya ukaguzi wa ndani na itaundwa kuanzia mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa hivyo, ongezeko hilo la fedha linatokana na mishahara ya watendaji wa idara hiyo mpya ambayo inakisiwa kwamba itafikia shilingi bilioni mbili, milioni mia tisa arubaini na nne.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hassan Khamis Hafidh alizungumzia kuhusiana na suala la fidia kwa walioanguka katika mikarafuu. Mhe. Naibu Spika, suala hili tunalichukua tutafanya jitihada maalum za kuhakiki taarifa zote za madai ya fidia hizo, serikali nieleze kwamba imeshalipa madai yote ya fidia ya miaka ya

nyuma, miaka michache iliyopita. Haya kama yapo madai mengine mapya tutayafatilia, tutayahakiki na tutajitahidi madeni yote hayo yenye usahihi yalipwe hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Agosti mwaka huu, basi madai hayo yote yawe yameshalipwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu bima, kwa mujibu wa mikataba ya bima mwananchi na yeye anayo haki ya kulipwa fidia baada ya kupata ajali. Shirika la Bima la Zanzibar linapokea ithibati kutoka Mahakamani baada ya kumaliza kesi na kujuulikana nani mkosa kati ya chombo au mwananchi. Iwapo Mahakama itaamua kuwa mwananchi hakuwa na kosa katika ajali, mwananchi huyo analipwa fidia, na iwapo mwananchi huyo atafariki basi malipo hayo yanalipwa kwa warathi wake. Kwa hiyo, ndio utaratibu ulivyo kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, suala la uwekezaji kutoka nje na hata wa ndani ya nchi pia lilizungumzwa na Mhe. Hassan na ni vyema tukafahamu kwamba mchango wa *FBI* (*Foreign Directly Investment*) katika nchi zote duniani ni muhimu katika kuimarisha uwekezaji na uchumi wa nchi. Mifano mizuri inaonekana ile iliyotokea Dubai, nchi ya Singapore, Rwanda, Afrika ya Kusini, China na nchi nyengine kwamba fedha kutoka nje zimesaidia sana katika kujenga ile *capital information* ya nchi zile, lakini vile vile kuleta haiba nzuri na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi. Kwa Zanzibar zaidi ya asilimia 60 ya uwekezaji wa mitaji binafsi uliosajiliwa na *ZIPA* ni uwekezaji kutoka nje ya nchi, kwa maana *Foreign Directly Investment* ambao unachangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa ajira, mapato ya serikali lakini pia kupata teknolojia mpya na za kisasa na kuwa na uchumi mpana (*Economic Diversity*).

Bado Zanzibar kama nchi nyengine itaendelea kuwakaribisha wawekezaji kutoka nje kuleta mitaji yao ambayo ina faida kubwa sana katika nchi hii. Wawekezaji wa ndani nao wana umuhimu wa

pekee katika kuchangia uwepo wa miradi ya uwekezaji nchini. Serikali kupitia *ZIPA* na taasisi nyengine za umma na binafsi zitaendelea kuwashajihisha wazalendo kuekeza mitaji yao. Hata hivyo, wengi wao bado hawana mitaji ya kutosha na kuweza kuwa na sifa za kuekeza kupitia *ZIPA.*

Mhe. Naibu Spika, programu za mafunzo zitaendelea kutolewa kwa wajasiriamali wadogo wadogo ili kuwapa uwezo wa kitaaluma na kuwashajihisha kuekeza katika miradi mbali mbali ikiwemo ya kilimo, viwanda vidogo vidogo na kadhalika. Hata hivyo, kuna haja ya wananchi wetu kupitia vyombo vya kifedha na mabenki kuwapatia mikopo mikubwa ili wawe na mitaji ya kutosha ya kuweza kutekeleza miradi hiyo ya uekezaji. Hili serikali inalifanyia kazi na kuna sera maalum inatayarishwa na wizara inayohusika kwa ajili ya kuwasaidia na hata mfumo wetu wa kodi pia unazingatia maslahi ya wafanyabiashara wadogo wadogo na waagiziaji wadogo wadogo.

Mhe. Naibu Spika, serikali itaendelea kuunga mkono wananchi wake kwa kuwapa kipaumbele katika taratibu zote za uwekezaji na upatikanaji wa vibali na ruhusa kwa kufuata sheria za nchi. Hata hivyo, ushauri aliotoa Mhe. Hassan Khamis Hafidh kuhusu kuundwa kwa taasisi za kukusanya kodi na ya kufuatilia ulipaji kodi, nimwambie mheshimiwa na nimuhakikishie kwamba ushauri wake huu tunauchukua. Ni ushauri makini tutauzingatia ili tuwe na chombo maalum au kitengo maalum kitakachokuwa ingawaje kazi hiyo inafanywa, lakini kukiongezea nguvu kitengo hicho kwa ajili ya ufuatiliaji hasa ya wale walipa kodi ambao ni sugu na hawataki kufuata sheria katika kulipa malipo ya kodi zao.

Mhe. Naibu Spika, hiyo itakwenda sambamba na kushajihisha wakandarasi wazalendo nao kupata kazi. Lakini hapa niseme sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za serikali ya mwaka 2016 imeweka mazingira mazuri sana ya kuwasaidia wakandarasi wetu na *suppliers* wetu kuweza kushiriki katika utoaji wa huduma

mbali mbali zinazoendelea nchini. Kwa hivyo, wao washajihike kuchukua fursa hiyo iliyopo ili waweze kufaidika na kupata kazi katika serikali, lakini pia kazi katika sekta binafsi ikiwa ujenzi, ikiwa usambazaji wa vifaa na huduma mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia tutazingatia maslahi ya Wahasibu Wakuu na tutafanya tafiti kujua mahitaji ya barabara ambapo tayari kuna *master plan* ya barabara za ndani ambayo iko chini ya wizara inayohusika na masuala ya barabara lakini pia wizara ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Lakini utafiti utafanyika ili kuweza kujua ni njia zipi za ndani ambazo zipewe kipaumbele cha kwanza. Ulitaja na barabara yako ya jimbo lako Mheshimiwa la Welezo, nadhani utafiti huo utabainisha kama barabara hiyo itastahiki kupewa kipaumbele cha mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Abdalla Maulid Diwani alitaka kujua kwa nini *ZRB* inapata asilimia 5 ya makusanyo halisi ya mapato wanayokusanya, na kwa nini *TRA* hawapati, anasema basi angalau wangepata asilimia 2. Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo Mhe. Rashid Ali Juma amelieleza vizuri suala hili, lakini nizidi tu kusema kwamba *ZRB* ni chombo cha SMZ na hiyo asilimia 5 wanapewa kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa chombo chenyewe, wakati *TRA* ni chombo cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wao wana utaratibu wao mwengine wa kupata fedha za uendeshaji wa chombo hicho.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu boti iliyopakiwa mizigo katika bandari ya Malindi na kurejeshwa na kikosi cha KMKM. Suala hili pia lilizungumziwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub. Ni vyema tukubali kwamba wapo watu wasiotaka kufuata sheria za nchi na hutumia hela nyingi za kufanya biashara za magendo, hilo halina mjadala lipo na hao watu wapo. Naomba tuwapongeze sana askari wetu wa KMKM kwa kazi nzuri ya ulinzi wanayoendelea kuifanya katika nchi yetu. Kwa kawaida askari wanapoona jambo sio la

kawaida huingilia na kuhoji pale wanapopata majibu mazuri na yasiyotia shaka huwa hawana matatizo na wahusika. Boti hii kwa taarifa tulizonazo baada ya kuonekana inasafirisha mizigo ilifuatwa na chombo cha KMKM na kutakiwa kusimama jambo ambalo walikataa kutii amri hiyo ya askari na ndipo hapo askari wa KMKM walipopiga *blackow* na wala haikuwa risasi, na mlio wa *blackow* ni mdogo kuliko mlio wa risasi. Na zilipigwa *blackow* hizo kwa madhumuni ya kuwatisha na kusimama ili ijuulikane ndani ya chombo hicho kuna kitu gani, hicho ndicho kilichofanyika.

Lakini mara baada ya kusimama walitakiwa watoe vibali ya bidhaa walizonazo katika chombo. Kwa bahati mbaya sana kwa taarifa tulizonazo walikaidi kufanya hivyo, walipokaidi kutoa vibali hivyo ndivyo walivyotakiwa kurudi bandarini na walipofika bandarini walitoa hivyo vibali lakini pia *ZRB* ilibidi watoze faini kwa kukaidi amri halali ya askari. Kwa hivyo, tunachoweza kujifunza hapa ni kwamba tuwaambie tu waheshimiwa wananchi wetu muhimu sana kufata sheria za nchi, na pale sheria za nchi zinapofuatwa hakuna tatizo wala huna haja ya kumuogopa askari kama wewe huna makosa. Askari akikusimamisha kama huna makosa, huna matatizo, tatizo lako ni kusimama kumsikiliza anachokitaka, kumpa anachokitaka kwa maana ya hati na baada ya hapo ugomvi unamalizika. Lakini ukiendelea kubishana na askari, askari yupo kwa mujibu wa sheria na yuko pale kutekeleza amri sahihi ya serikali ya kuweka amani na utulivu katika nchi yetu.

Mheshimiwa malipo ya ujenzi wa fidia ya mitaro kwa wananchi wa Jang'ombe hili tayari nimeshaieleza, tayari wameanza kuitwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla alitupa ushauri na alitupa pongezi namshukuru sana tumepokea ushauri na pongezi zake. Lakini pia alitaka kujua tafsiri ya maneno "Mubashara"  na mimi nijibu kwa *context* ya hotuba yangu maneno "Mubashara" tulizungumzia ni

yale matangazo yanarushwa moja kwa  moja kwa maana *live* hiyo ndio maana tuliyoikusudia na nadhini Mheshimiwa mama yangu Panya Ali Abdalla atakubaliana na tafsiri yangu hiyo na hakutakuwa na tatizo kwenye hilo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said nakubaliana nae kuhusu umuhimu wa kudhibiti matumizi ya serikali na kudhibiti upotevu wa mapato ya serikali. Ni jambo ambalo serikali hivi sasa linalifanyia kazi kwa nguvu zote. Aidha, elimu kwa walipa kodi inatolewa na itaendelea kutolewa na kuimarisha utaratibu wa sekta binafsi na Wizara ya Fedha katika kukuza fursa za ajira na ulipaji wa kodi *electronically*  au ki-*electronic*.

Lakini Mhe. Suleiman Sarahan Said pia alitaka kujua hatma ya mtu mmoja ambaye alikuwa akiishi katika jengo linavunjwa kupisha ujenzi wa jengo la Shirika la Bima Zanzibar pale Chake Chake. Ameeleza kwamba mtu huyo ameishi katika jengo lile kwa zaidi ya miaka 28 na niseme tu kwamba wananchi hawa waliokuwa wakitumia jengo lile walikuwa wamekodi na taratibu za kuondoshwa baada ya jengo lile kutakiwa zimefuatwa. Lakini hata hivyo, shirika lilitoa chochote kwa baadhi yao na naamini kwamba walitoa wote lakini kama yupo mmoja kwa bahati mbaya hakupata nimuahidi Mhe. Suleiman kwamba tutalifUatilia na iwapo ni kweli kwamba yeye hakupata na wenzake wamepata chochote basi tutaangalia uwezekano na yeye wa kupatiwa hicho kitu kidogo.

Mhe. Maryam Thani Juma wa Gando yeye alizungumzia kuhusiana na soko la *ZUSP* Wete alieleza kwamba soko hili halijamilika na alieleza pia linavuja. Lakini nikiri kwamba soko hili tayari limezinduliwa na Mhe. Rais Dkt. Ali Mohammed Shein na lilizunduliwa wakati wa sherehe za miaka 53 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Niseme kwamba tutalifatilia kwa kushirikiana na Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum ambao ndio wasimamizi wa jengo lile. Lakini

pia kuna hili suala zima la kwamba soko hilo halijaweza kuanza kutumika, nalo tutaliangalia kujua kuna changamoto gani zinazosababisha matumizi ya soko lile.

Kuhusiana na soko jengo la Hoteli ya Wete, jengo la hoteli ya Wete hili tayari serikali imelitoa kwa Benki ya Watu wa Zanzibar na tayari benki imeshatayarisha michoro yake na imeshapata mkandarasi kwa maana mkandarasi huyo anajulikana kwa jina la *Zege Construction* na hivi karibuni watanza kwa ujenzi wa paa na baadae waende na kazi ya kulikarabati jengo hilo.

Kuhusiana na Jengo la Sinema la Wete nalo jengo hili liko chini ya Idara ya Utamaduni na limekodishwa kwa Ndg. Ali Khamis kwa umarufu Roki toka mwaka 2014 na mkataba wake unamalizika mwaka 2017. Masharti aliyopewa aliyekodi ni kwamba aendeleze kuonesha sinema katika jengo lile.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Miraji Khamis Mussa alisisitiza sana juu ya suala la umuhimu wa kuweka kumbukumbu za ukodishaji wa serikali na uwekaji wa *asset register***.** Suala hili pia lilizungumziwa na Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi nimuelezee na niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe kwamba kazi ya kuandaa *asset register* kwa kila wizara inafanyika na tayari wizara tano zimeshakamilisha zoezi hili wizara nyengine zinaendelea na zitaendelea ndani ya mwaka wa fedha 2017/18.

Kuhusiana na suala la kukaguliwa kwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Hivi sasa Mfuko Mkuu wa Serikali unakaguliwa ni kweli huko nyuma Mfuko Mkuu wa Serikali ulikuwa haufanyiwi ukaguzi. Lakini kuanzia mwaka wa Fedha 2016/17 mfuko mkuu unafanyiwa ukaguzi na taarifa yake itapatikana.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu malipo ya *VAT* na Ushuru wa Bidhaa kwa malipo ya huduma za simu, TV za kulipia na huduma za fedha nimjulishe Mhe. Miraji Khamis Mussa Mswada wa Sheria

unaotarajiwa kuwasilishwa hapa Barazani katika kikao hiki utaweka utaratibu mzuri wa sheria wa kutoza kodi hiyo hapa Zanzibar. Ushuru wa bidhaa zinazoingia nchini kutoka nje ya nchi na huduma kwa maana ya *service* si jambo la Muungano na hivyo Zanzibar itaweka sheria yako kutoza kodi hiyo.

Hata hivyo, kwa miamala ya ki-*electronic* kwa makampuni ya simu na mabenki hivi karibuni kama tulivyoona Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alizindua mfumo wa ki-*electronic* wa ukusanyaji wa kodi *Electronic Revenue Collection System*. Mfumo ambao umeandiliwa kwa mashirikiano ya pamoja baina ya *TRA* na *ZRB* na utatumika pande zote mbili za za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kodi ile inayostahiki kuja Zanzibar, basi mfumo ule unatambua moja kwa moja kodi hizo na moja kwa moja zitapelekwa kwenye *account* ya *ZRB.*

Kwa ile miamala ambayo itafanyika kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania basi fedha zile moja kwa moja zitapelekwa katika *account* ya *TRA* ambazo zipo Benki Kuu. Kwa hivyo, hakuna matatizo na mfumo huu ni *automated* hakuna *human entervision* na hakuna mtu atakaeingilia unakwenda *automatically*. Kwa hivyo, ni mfumo mzuri na sisi tunaufurahia na tunadhani pia huko mbele tuwe na utaratibu wa kuunganisha huduma nyengine katika mfumo kama huu ili tuweze kukusanya mapato yetu kupitia mfumo wa ki- *electronic*.

Mapato ya Uhamiaji wanakusanywa Zanzibar wanabaki Zanzibar na kutumika Zanzibar kwa kamubaliano baina ya serikali zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *VAT* inayotokana na huduma ya Posta inalipwa na zinatozwa *VAT* huduma hizo na zinalipwa hapa hapa Zanzibar na kwa wastani tunapata baina ya milioni 4.5 hadi milioni 5 kwa mwezi. Lakini hii hatujaweza kutenganisha kile kima halisi kinachopatikana kutokana na

huduma za kiposta. Nalo tunalichukuwa tutakwenda kulifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, suala la kukusanya kodi kwa wawekezaji wanaouziana na kubadilisha umiliki. Sheria ya Ushuru wa *Stamp* ya mwaka 1996 ilikuwa haijaweka utaratibu mzuri wa uhaulishaji, ila sheria mpya inayopendekezwa ambaye itawasilishwa katika kikao hichi itaweka utaratibu mzuri zaidi wa kusimamia suala hili.

Aidha sheria ya Usimamizi wa kodi kwa maana ya *Tax Administration Procedure Act* ya mwaka 2009 imeweka utaratibu katika kifungu cha 54(a) wa kudhibiti mauziano na *management fees* katika marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2016. Uhaulishaji unaofanywa nje ya nchi bila ya kufata taratibu za sheria za nchi unakuwa batili na haukubaliki lazima mradi huo utape usajili na kulipa kodi zinazostahiki hapa nchini.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Miraji Khamis Mussa pia alitaka kujua iwapo mgao unaotokana na mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu unapatikana na taasisi gani inayokusanya fedha hizo. Naomba nimjulishe Mhe. Mwakilishi kwamba mgao huo upo kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ya kuwa asilimia 50 ya mapato yanatumika kwa gharama za uendeshaji wa mamlaka na asilimia 30 yanakwenda kwenye Hazina Tanzania Bara na asilimia 20 yanabaki kwenye Hazina Zanzibar. Fedha hizi kwa hapa Zanzibar zinakusanywa na Bodi ya Mapato ya Zanzibar na kwamba kwa mwaka 2016/17 jumla ya shilingi milioni mia nne na thamanini zimepatikana.

Mhe. Ali Khamis Bakar alizungumzia kurundika kwa vifaa vichakavu na alitaka kujua utaratibu gani uliopo katika kuondoa vifaa kama hivyo. Nimjulishe tu kwamba ununuzi na uondoshaji wa vifaa vichakavu vya serikali unafanywa kwa mujibu wa sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali ya serikali mali ya umma ya mwaka 2016 na utaratibu ni kwamba taasisi inayohusika ndio

inayohusika na uondoshaji wa mali hiyo. Lakini huwa inaomba ridhaa ya Wizara ya Fedha, kwa hivyo, wanawaandikia Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha inafanya tathmini na baada ya kufanyika tathmini hiyo basi vifaa hivyo huondolewa mara nyingi huondolewa kwa mnada wa wazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub alizungumzia suala la mizigo inayota Zanzibar na kwenda Tanzania Bara na kadhia iliyopo. Hili tumeshalizungumza mara nyingi na tulisema hata juzi nililitolea ufafanuzi kwamba litatokana na kuwa na mifumo miwili tafauti ya kutathmini mizigo na bidhaa hizo. Hapa Zanzibar bado tunatumia *Skuda Plus Plus* wakati wenzetu Bara wanatumia *Tanzania Custom Integrated System (TCIS).*

Sasa mifumo hiyo miwili ndiyo inayoleta utafauti huo na kwa wenzetu Bara walikuwa wanataka hili suala liwe *centralized* na sisi tuna *reservation* yetu katika baadhi ya maeneo. Kwa hivyo, tunaendelea kujadiliana baina ya wizara zetu mbili ili kuweza kupata muafaka katika suala hilo.

Suala la *ZSFF* kuwaachia jengo Idara ya Ujenzi, niseme pale Michezani waendelee kukaa. Maelekezo ya serikali tayari yameshatolewa na pale watu wote wameshatakiwa kuondoka pamoja na wao na wao serikali itawatafutia mahala pa kuweza kukaa kwa kuendesha shughuli zao. Kwa hivyo, hili ni suala la serikali maamuzi yameshatoka na linafanyiwa kazi.

Suala la boti iliyorejeshwa tayari nimeshalitolea maelezo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maeelezo hayo naanimi kwamba nimejitahidi kwa kadiri ya uwezo wangu. Lakini kama yapo maeneo ambayo sikuyagusa basi wachukulie tu kwamba tumeupokea ushauri wao tumeuchukua na tutayafanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kukuulizeni kuhusiana na kukubali hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na kutizama muda kwa sababu tunatakiwa leo tuimalize wizara hii. Ni matarajio yangu kwamba inawezekana zikazidi kama dakika kumi katika kupitisha vifungu. Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri katika Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais atengue kanuni ya hoja ya wakati ili tuweze kupata kama dakika kumi nyengine kwa ajili ya kuendelea na kupitisha vifungu. Mheshimiwa waziri karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kwa mujibu wa orodha ya shughuli za leo muda uliopo haututoshi kukamilisha suala zima la kupitisha Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo naomba tuweke kando kanuni 23(1) ya muda ili tuweze kumalizia shughuli iliyo mbele yetu.

Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kwa Baraza lako tukufu tuweke muda wa kanuni kando ili tumalizie shughuli iliyo mbele yetu mpaka hapo tutakapomaliza kupitisha Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Naibu Spika, naafiki

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri ametoa hoja sasa niwaulize, wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

Sasa Waheshimiwa Wajumbe tunarudi tena katika hoja ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na niwaulize, Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja hii wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Naibu Spika, naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

## KAMATI YA MATUMIZI

## FUNGU F01 - WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

**Jumla ya Mapato** **<u>1,060,919,471</u>**

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu PF0101 Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii nilikuwa nataka maelezo za ziada kuhusu ufafanuzi alioutoa Mhe. Waziri. Lakini ki msingi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa ufafanuzi wake.

Nilikuwa nataka maelezo ya ziada kuhusu ile kadhia niliyosema ya wananchi ambao baadhi yao ni wapiga kura wetu ni wote wapiga kura wetu ambao walipata kadhia ya kusimamishwa katika ule upotevu wa fedha uliofanyika katika Wizara ya Fedha. Nafikiri Mhe. Waziri mimi nilisema wafanyakazi waliosimamishwa ni watano lakini inaonesha ni zaidi ya watano.

Lakini sasa amesema kwamba katika uchunguzi ule kumeonekana kuna wengine zaidi ya 21. Lakini mimi hoja yangu iko kwamba wale ambao wameliosimamishwa karibu mwaka mmoja sasa hivi ni watu watano na ambao wanakula nusu mshahara. Lakini hao wengine wote ambao walionekana wanahusika wao bado wanapo kazini na waneendelea kula mshahara kamili. Sasa hapa ndio hoja yangu inapokujwa kwamba mbona hapa haki haitendeki.

Kwa sababu kama kuna kosa limefanyika na kuna tume imeudwa na ile tume bila shaka imeshawasilisha ripoti na kama imewasilisha ripoti kama wale wanaonekana wamehusika ilikuwa hatua za kinidhamu zichukuliwe. Lakini mpaka sasa hivi wanaoadhibika ni watu wachache wengi bado wako kazini. Sasa nilikuwa nataka maelezo ya zaida katika hili Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Hamza Hassan Juma suala lake kuhusiana na kadhia inayowahusu wafanyakazi waliosimamishwa kazi.

Ni kweli kwamba wako wale waliosimamishwa kazi pale tuhuma ilipotokea na hilo ni jambo la kawaida na wakati uchunguzi unaendelea unaweza kubaini wengine zaidi. Kwa hivyo, baada ya kubainika wengine zaidi nao waliunganishwa na wao pia walipewa barua zao kwa siku ile ambayo walibainika. Lakini hata sasa hivi suala hili likipelekwa katika mashauri ya mahakama ikitokezea wako wengine watatajwa ndani ya kadhia hiyo na wao watakuja kuunganishwa wakati huo watakaotajwa. Kwa hivyo, suala la muda lini inatokea kutokana na hali halisi ya uchunguzi

unavyoendelea na shughuli yote hii inafanyika kwa mujibu wa sheria namba 2 ya mwaka 2011 ya Utumishi wa Umma.

Hata hawa ambao wamechukua muda bado tunasema kuna kipengele cha sheria hiyo kinachoelezea kwamba wanasimamishwa kwa miezi sita ya mwanzo. Lakini vile vile unaweza kuwasimamisha kwa miezi sita mingine ikiwa suala lile bado halijapatiwa ufumbuzi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe akubali kwamba suala hili liko katika mikono ya kisheria linafanyiwa kazi vizuri na wala hakuna wasiwasi, hakuna hata mfanyakazi mmoja atakayenyimwa haki yake ya kwamba hahusiki akaingizwa katika kadhia.

Vile vile nilitoa maelezo Mhe. Mwenyekiti, kwamba mfanyakazi mmoja ambaye aligundulika hakuwemo katika kadhia ile kwa sababu hakuweza kuunganishwa, huyo tayari ameshakuwa *reinstated* amesharejeshwa kazini.

**Mhe. Mwenyekiti:** Wengine mlikuwa hamjanyanyuka. Mwanzo kabisa kwa utaratibu mnanyanyuka nyote halafu nawatajeni nyote. Aliyesimama ni Mhe. Hamza Hassan Juma peke yake wengine hamkunyanyuka. Mhe. Hamza endelea.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani Mhe. Waziri amejaribu kutoa maelezo, lakini bado hoja yangu iko pale pale. Sheria aliyoitaja waliyosimamishwa wale ni sheria ya Utumishi wa Umma. Lakini pia kuna hii sheria ya fedha ambayo tuliyoipitisha hapa hapa, sheria ya mwaka 2005 ambayo pia nayo ilikuwa inasimamia haki za wafanyakazi hao hao. Ukiangalia sheria ya fedha ya mwaka 2005 nilijaribu kunukuu kifungu cha 22 kinasema:

"Kunapotokea hasara yoyote katika hesabu za serikali wakuu husika wa *vote* zinazohusika, yaani Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi hutakiwa kutoa maelezo kwa

Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, na *copy* kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, yaani *Pay Master General*.

Je, hapa kuna Makatibu Wakuu wangapi ambao waliotoa hizo taarifa za upotevu wa fedha na mpaka ikachukuliwa hatua kama hiyo.

Lakini vile vile isitoshe Mhe. Mwenyekiti, hao ambao waliosimamishwa,walipewa barua ya kusimamishwa pale mwanzo, mpaka nakuja na taarifa hii walikuwa bado hawajapewa taarifa ya kuongezwa hiyo *extension* ya miezi sita ya kusimamishwa kwao na ndio maana hawa wakawa wanaishi mitaani wanahangaika hawajui nini kinachoendelea. Sasa labda ningepata maelezo ya ziada.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba Mhe. Hamza Hassan aelewe kwamba sikujaribu kutoa maelezo, nilikuwa natoa maelezo ambayo nina uhakika nayo, na nitaendelea kusimamia kwenye maelezo hayo, kwa hivyo sikujaribu.

Mhe. Mwenyekiti, ninachokieleza ni kwamba sheria ya fedha kama kainukuu ile ya mwaka 2005, ndio iliyotumika katika kuunda bodi ya uchunguzi *board of inquiry* iliundwa kwa mujibu wa sheria hiyo, lakini watumishi wote wa umma wanatawaliwa chini ya sheria namba 2 ya mwaka 2011 ya Utumishi wa Umma, ambayo hiyo ndio iliyofuata.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la kuongezewa muda ndani ya kifungu cha sheria haikulazimisha kwamba mfanyakazi anapopewa barua ya kusimamishwa kazi katika kipindi cha mwanzo cha miezi sita kwamba ni lazima apewe barua tena ya kuongeza muda huo wa miezi sita mingine, hilo halipo wazi katika sheria. Lakini hili suala la makatibu wakuu tuliunda bodi.

Kwanza niseme katika hoja yake ya mwanzo Mhe Hamza Hassan hilo halikuwemo la kwamba Makatibu Wakuu, ama walijulishwa, hilo halikuwemo wala hakuonesha *indication* ya kwamba atalisimamia suala hili. Lakini pamoja na hayo ile bodi ya uchunguzi iliyofanya kazi ndio iliyotuletea maoni na *observation* zao, na wakatoa na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa kwa wale wahusika. Hakuna Katibu Mkuu hata mmoja aliyeainishwa katika ripoti ya *board of inquiry.*

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Unajua Mhe. Mwenyekiti, sitaki twende kwenye kura, lakini nilikuwa nataka tu busara kidogo itumike kwa sababu unajua hapa kuna watu sasa hivi wanatumikia adhabu na watu wanapotumikia adhabu kitu kitakachowaokoa peke yake ni sheria ambazo tulizozipitisha. Ndio maana mimi baada ya kujenga ile hoja jana nikajaribu kuangalia, kwa sababu unajua unapojenga hoja basi unajaribu kuangalia *angle* tofauti tofauti, ndio maana nikajaribu kuangalia ile sheria ya fedha nikaona kifungu cha 22 kile kilikuwa kinatoa ufafanuzi hasa katika masuala ya upotevu wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sasa kwa kuwa sitaki niende mbali sana na kwa sababu tayari nilikwisha kuangalia, hata kifungu cha 8(1) cha sheria hiyo hiyo ya fedha ya mwaka 2005 kinaeleza kwamba fedha yoyote itakayotumika katika *vote*, *Accounting Officer* ndiye mwenye dhamana ya fedha hizo, na kanuni namba 11 ya sheria hiyo inafafanua dhamana ya huyo Afisa Uhasibu yaani *Accounting Officer*.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kitu kimoja, na ndio maana nikasema sitaki twende kwenye kura. Mimi hili fungu nitaliruhusu, lakini naomba sana Mhe. Waziri mimi ambaye niliyejenga hii hoja naomba baadae tuje tukae anifafanulie vizuri ili tuangalie hii haki ya hawa wananchi wetu inapatikana vipi. Kwa sababu kama hizi sheria mbili, Sheria ya Utumishi wa Umma na Sheria ya Fedha kama zinatofautiana katika utekelezaji

wake, mimi nafikiri hawa wafanyakazi wetu wataendelea kusota muda mrefu nje, lakini vile vile wenzao wanaendelea kufurahia maisha ndani ya taasisi zao. Kama upotevu wa fedha Mhe. Mwenyekiti, kule Wizara ya Fedha wale ni watoaji tu wa fedha, lakini watumiaji wa fedha wanakuwa katika taasisi nyengine. Sasa ndio maana nikasema kwamba anayehusika hapo ni *Accounting Officer*, fedha ikishatoka Wizara ya Fedha inakwenda kwa Katibu Mkuu halafu yeye Katibu Mkuu wa Wizara ndio ana-*disburse* katika taasisi zao. Lakini sasa leo kule wameng'ang'ania watu wa Wizara ya Fedha ambao wao ni *distributor* tu wa zile fedha.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hii suala mimi nahisi kama kidogo lina utata, au labda Mhe. Mwanasheria Mkuu anaweza akatusaidia hizi sheria za fedha na sheria hii ya utumishi wa umma zinaelekeza vipi katika masuala kama haya yanavyotokea. Lakini pia hata hii bodi iliyoundwa Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa inakuja na mapendekezo.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe Hamza Hassan Juma maliza, imekuwa sasa unachangia.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Sasa hii bodi ambayo imeundwa na Mhe. Waziri, ndio iliyotoa mapendekezo kwamba hawa watu wapelekwe mahakamani, labda nipate ufafanuzi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Hamza Hassan Juma umetoa wazo zuri kabisa, la kusema tuipitishe halafu baadae utakaa na Mhe. Waziri. Kwa hivyo, baadae utapata ufafanuzi wa ziada kwa Mhe. Waziri. Umetoa wazo zuri kabisa, nafikiri ni zuri na ninamuomba Mhe. Waziri akubali kukaa na wewe baadae ili akupe ufafanuzi wa ziada. Ahsante Mhe. Hamza tunakushukuru. *(Makofi)*

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kusimamia maelezo ya sheria. Mhe. Mwenyekiti, ni vyema tuwe

waangalifu sana na hasa tunapolizungumza jambo hili ambalo na wahusika wenyewe wanasikiliza. Kadhia hii bado kama alivyosema Mhe. Waziri iliundiwa tume na hiyo tume imekuja na mapendekezo yake lakini haikumalizika, bado inaendelea kufanyiwa kazi. Sasa tukianza hapa kugeuka sisi ndio chombo cha kujadili mambo ambayo bado hayajaamuliwa, mimi nadhani hatutotenda haki Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Ni vyema sana Mhe. Mwenyekiti, tuziwache taratibu za kisheria zifanye kazi yake, zitakapomaliza hawa ambao watahusika basi wana wajibu wa kwenda mahakamani na wale ambao hawatohusika basi wataachiwa waendelee na shughuli zao. Lakini tukianza kuanza kujadili jambo hili ambalo bado kadhia yake haijamalizika, mimi sidhani kama itakuwa tunajenga haki kwa wale ambao wako nje wenye kadhia hii, na sisi kama serikali ambao tunatakiwa tutoe maamuzi. Mimi nadhani Mhe. Hamza Hassan keshajenga hoja yake. Hoja yake anasema kwamba kwa nini Makatibu Wakuu hawakuingizwa, na Mhe. Waziri ameshajibu kwa nini hawakuingizwa, kwa sababu hiyo kamati iliyoundwa haikuja na mapendekezo yao. Kwa hivyo, sio vyema ku-*disclose* hapa taarifa ya kamati ambayo bado serikali haijaitolea maamuzi yake, mimi nadhani hatutokuwa tunafanya haki Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Nafikiria ni vile vile ambavyo… Mhe. Hamza Hassan Juma kaa kitako kwanza, nakuomba ukae.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, kalirejesha Mhe. Mwanasheria Mkuu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Hamza Hassan Juma nakuomba ukae, kuna jambo na mimi nataka kusema, na mimi nina haki ya kuzungumza au vipi. Nasemaje, yeye ametoa ufafanuzi wa kisheria na utaratibu ambao unatumika katika kumaliza hili suala, ndilo alilosema Mhe. Mwanasheria Mkuu. Mimi nasemaje...

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Hoja yangu Mhe. Mwenyekiti, yeye alisema kwa kuwa suala hili limeundiwa tume halijamalizika. Sisi jambo ambalo tunalokatazwa kulizungumza ni jambo lililokuwepo mahakamani. Lakini jambo ambalo liko ndani ya serikali tunayo haki ya kulizungumza. *(Makofi)*

Lakini bado mimi nasikiliza ule ushauri wako kama ulivyomuelekeza Mhe. Waziri wacha tukae tulifuatilie suala hili. Sisi haja yetu haki itendeke, hakuna hata mwakilishi mmoja humu anayependa fedha za umma zipotee, lakini kitu ambacho tunakita ni haki itendeke. Kama kuna mtu kakosa ahukumiwe, lakini kama kuna mwengine kakosa na yeye vile vile ahukumiwe.

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu PF0101 | Usimamizi wa Bajeti na Fedha za Umma | 64,808,097,000 |
| Kifungu PF0102 | Programu Kuu ya Usimamizi na Uwekezaji wa Mali za Umma | 9,515,091,000 |
| Kifungu PF0104 | Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara Fedha na Mipango | 34,544,609,000 |
| | **Jumla Kuu** | **108,867,796,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima*
*bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU F02 - MFUKO MKUU WA SERIKALI**

| | | |
|---|---|---|
| Kifungu PF0201 | Programu Kuu ya Usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Serikali | 101,108,000,000 |
| | **Jumla Kuu** | **101,108,000,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU F03 - TUME YA MIPANGO**

| | |
|---|---|
| Kifungu PF0301 | Programu Kuu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi |

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, leo Katibu Mezani anatupata kweli kweli, maana yake waheshimiwa wakitaka kusimama kishapita. Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye hoja yangu. Hoja yangu katika masuala mazima ya mipango yetu ya kitaifa na nilizungumzia sana suala zima la maeneo ambayo yamekaa muda mrefu bila ya kuwekezwa na ni maeneo ambayo ni ya uekezaji.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru kwanza Mhe. Waziri kwa sababu hiyo kazi tayari alikwishakuipa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira lakini kuna hoja ambayo iliyokuja nilipozungumza suala la Kiwanda cha Nondo. Mhe. Mwenyekiti, kiwanda nilichokizungumza mimi cha nondo sio kiwanda kikubwa, ni *Light Industry.* Hata pale Dar es Salaam hao wawekezaji wanacho kiwanda kipo katika maeneo ya *Light Industry*. Kwa sababu wao uwekezaji wao ulikuwa unachukua hekari 10 tu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kuna maeneo mengi ambayo ni ya uwekezaji ambayo yapo hayatumiki kwa muda mrefu yanashindwa kuendelezwa.

Sasa labda Mhe. Waziri angejaribu kunitolea ufafanuzi, kwa sababu hicho kiwanda nilichozungumza mimi sio kile cha wale

Waholanzi waliokuja, lakini hao ni Watanzania ni wananchi wazalendo ambao hawa...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Hamza Hassan Juma uliza swali, unatoa maelezo marefu.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Kiwanda chao wao ni *Light Industry*, sasa labda nipate ufafanuzi.

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Mwenyekiti, wakati nikitoa maelezo, nilieleza kwa nini ombi hili halikukubalika kwamba kiwanda hichi kiwepo katika eneo la Fumba. Kwa mujibu wa Fumba *master plan* ni eneo ambalo limetengewa hekta 100.2 na viko viwanda vya aina vilivyowekewa na kukubalika kuwekezwa katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini bado nilitoa maelezo ya kwamba kiwanda hiki ni muhimu, kama bado wana hamu na nia ya kuendeleza uwekezaji huu basi tuwasiliane na wizara husika iangalie eneo muafaka na upo utaratibu mzima ambao unafuatwa wa kupatiwa maeneo ya uwekezaji. Wapeleke *Letter of Intent ZIPA*, *ZIPA* watawasiliana na wizara inayohusika na masuala ya ardhi, baada ya taasisi zote zinahusika kukaa pamoja na kuujadili mradi huo. Lakini kwa eneo la Fumba kwa mujibu wa *master plan* kiwanda cha aina hii hakitokuwa na nafasi katika lile eneo la hekta 100, lakini kinaweza kupata nafasi katika maeneo mengine kwa kufuata utaratibu unaofuatwa na wawekezaji wengine.

**Mhe. Hamza Hassan Juma:** Mhe. Mwenyekiti, nafikiri watu wa *ZIPA* wangekuwa na maelezo mazuri kama ya Mhe. Waziri, basi hili suala wala lisingefika hapa. Kwa sababu mwekezaji ameshakuja sasa hivi zaidi ya miezi 9. Kama *ZIPA* wangetoa barua kama hiyo ya kwenda Wizara ya Biashara, mimi nafikiri hilo suala tungekuwa tumeshafikia pahala.

Lakini kwa kuwa ni hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tutawasiliana na wale wahusika waandike tena barua *ZIPA*. Lakini *ZIPA* sasa naomba wasicheleweshe kuwajibu wale wawekezaji wawaelekeze pale pahala pa kwenda. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante tunaendelea.

| | |
|---|---|
| Kifungu PF0301 | Programu Kuu ya Kuratibu Mipango ya Kitaifa na Maendeleo ya Watendakazi 1,516,237,000 |
| Kifungu PF0302 | Programu Kuu ya Usimamizi wa Uchumi Mkuu na Takwimu 6,191,400,000 |
| Kifungu PF0303 | Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Mipango 1,723,200,000 |
| **JUMLA KUU** | **9,430,837,000** |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Baraza Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Baraza lilirudia)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, tukae. Mhe. Waziri. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango:** Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara ya Fedha na Mipango bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ameshatoa hoja. Sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naiubu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Vile vile niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe, kwa michango yao mizuri. Pamoja na hilo basi tuitakie wizara hii utendaji au utekelezaji uliotukuka kabisa na kila la kheri.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa katika ratiba yetu kesho tutaendelea kuwa na shughuli za Baraza na kwa kuwa kanuni zetu zinasema kwamba shughuli za Baraza huwa zinakuwa siku ya Jumatatu mpaka Ijumaa. Hivyo, nitamuomba Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atengue kanuni ili tuweze kesho kuja kuendelea na shughuli zetu za Baraza. Mhe. Waziri karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 88(c) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, miongoni mwa kazi za Baraza la Wawakilishi ni kuuliza maswali kwa serikali. Kwa kuwa orodha ya maswali kwa serikali bado ipo kubwa. Kwa hivyo, naliomba Baraza lako tukufu kuweka kando kifungu cha 23 cha kanuni za muda wa Baraza, ili kesho siku ya Jumamosi tarehe 10/06/2017 saa 3:00 barabara za asubuhi tuweze kuendelea na shughuli za Baraza ili tuweze kukamilisha kazi hiyo ya maswali. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja. Sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo

wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

*Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru tena kwa shughuli yetu hii ya leo na hadi kufikia hapa ninaakhirisha kikao mpaka kesho saa 3:00 asubuhi

*(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 10/06/2017 saa 3:00 za asubuhi)*